# Nipashe

Jumatatu Agosti 19, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580000

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US



ST.JOSEPH UNIVERSITY In Tanzania


"WHERE YOUR DREAMS ARE NURTURED"

Calling all Old Students of SJCET, SJCIT, SJCMC, SJCHS and SJUIT-ARUSHA

SJUIT invites its Alumnus for the Alumni meet from 4:00PM-9:00PM on **24th August, 2019,** "Entrance is free". For details **www.alumni.sjuit.ac.tz**

For more information contact: +255 676 504 147 +255 745 281 505

215359802

## NGO 158 zaondolewa kwenye rejista ya msajili

UKURASA 4

# Wakuu SADC watoka na maazimio mazito

• **Ni** baada ya mkutano wao wa siku mbili kufungwa jana na kukubaliana kuwa...*Endelea uk. 2&3*



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Rais John Magufuli, akiagana na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa na Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob, baada ya kufunga rasmi Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**SERIKALI YAAGIZA KAMPUNI KULIPA USHURU MGODINI**

KAMPUNI tanzu mkoani Geita zinazofanya kazi ya kutoa huduma katika kampuni ya uchimbaji madini ya Geita Gold Mining...

UKURASA WA 26

**WALIOFARIKI AJALI YA MOROGORO WAFIKIA 95**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kufuatia ajali ya moto wa lori la mafuta iliyotokea Morogoro Agosti 10, imeongezeka...

UKURASA WA 26

**MWANAFUNZI KIDATO 2 AJIUA KWA RISASI**

MWANAFUNZI wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Meru ya jijini Arusha, Faisal Ibrahimu (19) mkazi wa Kata ya Kati mkoani...


## Kitanzini kukutwa na dhahabu bandia

UKURASA 4



RIPOTI MAALUM

## Madereva wazembe wanavyowamaliza Watanzania

UKURASA 4


**MICHEZO** USAJILI SPRITE BBALL KINGS 'WATETEMESHA' UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6




# Wakuu SADC watoka na maazimio mazito

**Na Gwamaka Alipipi**

MKUTANO wa 39 wa Jumuiya ya Nchi Kusini mwa Afrika (SADC) umemalizika jana jijini Dar es Salaam, huku wakuu wa nchi za jumuiya hiyo wakitoa maazimio ambayo yataleta manufaa kwa nchi wanachama.

Mkutano huo ulioanza kwa maonyesho ya viwanda Agosti 5, mwaka huu na juzi na jana ulihitimishwa kwa wakuu wa nchi hizo kukutana na kujadiliana baadhi ya ajenda kisha kutoka na maazimio hayo.

Wakuu hao ni kutoka Zambia, Afrika Kusini, Angola, Msumbiji, Lesotho, Eswatini, Tanzania, Malawi, Namibia, Zimbabwe, Botswana, Madagascar, Mauritius, Seychelles, Comoro, na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza wakati wa kufunga mkutano huo jana, Rais John Magufuli ambaye ni mwenyekiti mpya wa SADC baada ya kuchukua mikoba kutoka kwa Rais wa Namibia, Dk. Hage Geingob, alitaja ajenda na maazimio yaliyofikiwa na wakuu hao.

"Mkutano ulikuwa na ajenda na maazimio yaliyofikiwa na wakuu wa nchi, tumejadiliana ajenda nyingi na tumefikia maafikiano, endapo yakitekelezwa yataleta manufaa mengi kwa wanachama," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alisema katika kukuza sekta ya viwanda katika nchi za SADC, Mkutano umewahimiza nchi wanachama kuendelea kutekeleza mkakati na mwongozo wa maendeleo ya viwanda wa SADC wa mwaka mwaka 2015.

"Mkutano wetu ulifanyika katika kaulimbiu isemayo: Mazingira wezeshi ya kibiashara kwa maendeleo jumuishi na endelevu kwa viwanda na kukuza ajira, kauli mbiu hii ni endelevu kwa mikutano mingine ya SADC iliyofanyika Zimbabwe mwaka 2014, Botwsana mwaka 2015, Eswatini mwaka 2016, Afrika Kusini mwaka 2017, Nambia mwaka 2018," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Zote ziliweka mkazo kwenye utekelezaji wa mkakati mpango mwongozo wa kuendeleza viwanda ndani ya SADC wa mwaka 2015 hadi 16."

Alisema kaulimbiu ya mwaka huu imeweka msisitizo ya kuweka mazingira bora ya biashara ikiwamo kuondoa vikwazo mpakani, ukilitimba kwenye maamuzi na rushwa.

Rais Magufuli alisema ili kukuza sekta ya biashara katika ukanda wa SADC, wakuu wa nchi wameipitisha kaulimbiu hiyo na kuielekeza kamati kusimamia utekelezaji wake na kisha kuwasilisha ripoti kwenye mkutano ujao.

Alisema wakuu wa nchi wamesaini itifaki mbalimbali na lengo lake ni kuhakikisha maazimio kama vile ajira, kuendeleza viwanda yanafanikiwa kwa haraka zaidi.

Rais Magufuli alisema katika kikao cha wakuu walipokea ripoti ya mwaka kutoka kwa mwenyekiti wa SADC aliyemaliza muda wake pamoja ripoti ya mwaka kwa mwenyekiti anayemaliza muda wake wa Taasisi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya SADC.

"Wakuu wa nchi waliwapongeza wakuu hao kwa kazi nzuri walizofanya kwa mwaka uliopita," alisema Rais Magufuli.

**USALAMA WA DRC**

Alisema kwenye kikao chao wakuu wa nchi walikubaliana kuendelea kufuatilia suala la usalama nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

**MABADILIKO LESOTHO**

Alisema pia wameitaka Lesotho kuharakisha utungwaji wa sheria itakayoanzisha mamlaka ya kitaifa ya kusimamia mabadiliko.

**KUKABILIANA NA MAJANGA**

Alisema pia wakuu wa nchi wameiagiza kamati kuharakisha kuanzisha chombo za SADC cha kukabiliana na majanga, ambacho

INAENDELEA UK. 8



Madaraka Nyerere akiwaelezea wake wa marais kuhusu cherehani katika onyesho la 'Mchango wa Mwalimu Nyerere katika ukombozi wa Afrika'. Kulia kwake ni mama Janeth Magufuli, kushoto ni mke wa Rais wa Comoro, mama Azali Ambari na anayemfuata ni mke wa Waziri Mkuu wa Eswatini, mama Jane Dumile Dlamini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SADC yakubaliana mabadiliko ya sheria

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKUU wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jana, waliingia makubaliano ya pamoja na kufanya mabadiliko katika baadhi ya sheria, ikiwamo ya makosa ya uhalifu.

Pia wamekubaliana kulinda mimea na mazao yanayopatikana katika ukanda wa nchi za SADC.

Wakuu hao ni kutoka nchi za Zambia, Afrika Kusini, Angola, Msumbiji, Lesotho, Eswatini, Tanzania, Malawi, Namibia, Zimbabwe, Botswana, Madagascar, Mauritius, Seychelles, Comoro, na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), ambao walikuwapo nchini katika mkutano wa siku mbili.

Walisaini makubaliano kuhusu watuhumiwa watakaotenda makosa ya uhalifu katika moja ya nchi za SADC watapaswa kurudishwa nchini mwao na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria ya nchi yake.

Kadhalika, Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, alisaini makubaliano ya ushirikiano wa kudumisha masuala ya ulinzi, usalama na siasa.

Wakuu hao pia walisaini kwa pamoja makubalino ya uwapo wa manaibu makatibu watendaji wawili katika jumuiya hiyo, tofauti na awali aliyekuwapo mmoja.

Vilevile, Rais wa Msumbiji, Fillipe Nyusi alisaini makubalinao kwa nchi yake kukubali kulinda mimea na mazao yanayopatikana nchi za SADC.

# SADC, EU zasaini mkataba wa bil. 119/-

**Na Gwamaka Alipipi**

NCHI za Jumuiya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) jana ziliingia mkataba wa makubaliano na Jumuiya ya Ulaya (EU) wenye thamani ya Euro milioni 47 (Sh. bilioni 119.556), kusaidia programu tatu za maendeleo kwa muda wa miaka mitano.

Programu hizo ni kuboresha uwekezaji na mazingira bora ya biashara (SIBE), Programu ya kuwezesha biashara kufanyika kwa urahisi (TFP) na Programu ya kusaidia viwanda na sekta za uzalishaji (SIPS).

Katibu Mtendaji wa SADC, Stergomena Tax na Balozi wa EU, Jan Sadek, waliweka saini kwa niaba ya jumuiya hizo wakati wa kikao cha kuhitimisha Mkutano wa 39 wa Wakuu wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salam, kwamba Programu ya SIBE itasaidia upatikani wa ajira kupitia uwekezaji miongoni mwa nchi hizo.

Kwa mujibu wa Tax, TFP itasaidia kukuza na kuendeleza uchumi kwa nchi za SADC, wakati SIPS itasaidia nchi hizo kufikia malengo yake ya uchumi wa viwanda.

"Kuingia kwa makubaliano haya kumedhihirisha undugu uliopo kati ya SADC na EU, vile vile kutasaidia jumuiya hii kufikia malengo yake ya kuwa na uchumi bora kuwa na viwanda sambamba na upatikanaji wa ajira," alisema Tax. Vile vile, alisema programu hizo tatu zimehusishwa na zinaendana na kaulimbiu ya Mkutano wa 39 wa SADC isemayo: "Mazingira wezeshi ya kibiashara kwa maendeleo jumuishi na endelevu ya viwanda".

Kwa upande wake Balozi Sadek, alisema EU inaamini kuwa mazingira wezeshi ya kibiashara, uwekezaji na uboreshaji wa viwanda na kuweka mazingira bora kwa wafanyabiashara ndiyo njia pekee ya kufikia katika maendeleo.

Alisema programu hizo tatu zilizoingiwa makubaliano zinaendana na mtazamo wa EU katika kuzisaidia nchi za Afrika.

"Tunahitaji kusaidia mazingira ya kufanya biashara, kusaidia na kuboresha ufanisi wa kibiashara, kusaidia uwekezaji na viwanda kwa dhumuni la kukuza uchumi na upatikanaji wa ajira," alisema Sadek.

Ushirikano baina ya SADC na EU ulianza tangu miaka mingi, tangu miaka ya 2000 kiasi cha fedha kilichotolewa na EU kwa SADC ni Euro milioni 415 (Sh. trilioni 1.055) ambazo zilitumika katika kuboresha ulinzi na usalama, miundombinu, biashara, mazingira ya kufanya biashara pamoja na kilimo.




# Wake wa marais nchi za SADC wafurahia utalii Makumbusho

Na Mwandishi Wetu

WAKE wa Marais wa Umoja wa Maendeleo wa Nchi za Afrika ya Kusini (SADC) juzi walitembelea Makumbusho ya Taifa baada ya ufunguzi wa mkutano wa 39 wa nchi hizo, uliomalizika jijini Dar es Salaam jana na kujionea onyesho linalohusu mchango wa Mwalimu Nyerere katika ukombozi wa Afrika.

Wake hao wa marais wakiongozwa na mwenyeji wao Mama Janeth Magufuli, walitembelea Kijiji cha Makumbusho, Barabara ya Bagamoyo na Makumbusho Nyumba ya Utamaduni iliyoko mita chache kutoka ukumbi wa mkutano wa SADC.

Waliopata fursa ya ziara hiyo ni pamoja na Mke wa Rais wa Afrika ya Kusini, Dk. Tshepo Motsepe, Mke wa Rais wa Namibia, Monica Geingos, Mke wa Rais wa Comoro, Mama Azali Ambari na Mke wa Waziri Mkuu wa Eswatini, Mama Jane Dumile Dmlamini.

Kinamama hao walionekana kufurahia onyesho la Mchango wa Mwalimu Nyerere katika Ukombozi wa Afrika, ambalo mmoja wa waelezaji wa historia hiyo alikuwa mtoto wa Mwalimu Julius Nyerere, Madaraka Nyerere.

Kilichoonekana kuwafurahisha zaidi ni baadhi ya picha zilizobandikwa katika onyesho hilo ambazo na Madaraka alionekana akiwa mtoto.

Naibu Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, alimtambulisha Madaraka kwa wake hao wa marais na kusema kuwa inafurahisha zaidi kwamba historia ya Mwalimu Nyerere na mchango wake unaelezwa na mtoto wake ambaye mambo mengine alishuhudia kwa macho yake.

"Nani anaweza kueleza vizuri historia ya Mwalimu Nyerere kuliko mtoto wake mwenyewe? Angalieni na msikilize kutoka kwa mwanawe," alisema Naibu Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii.

Madaraka aliwaeleza na kuwaonyesha picha za familia yao ilijumuisha Mama Maria Nyerere na Mwalimu Julius Nyerere na watoto wao akiwamo yeye (Madaraka).

Eneo la onyesho hilo lilikuwa na cherehani, radio na Tv ya zamani walizotumia nyumbani kwao.

Wake wa marais walimuuliza maswali Madaraka na kufurahishwa na eneo hilo la onyesho.

Onyesho hilo linaonyesha juhudi za Mwalimu Nyerere katika ukombozi wa Afrika pamoja na alioshirikiana nao ikiwamo Samora Machel ambaye pikipiki aliyotumia katika kupigania uhuru imeonyeshwa katika onyesho hilo.

Pia wake hao walifurahishwa na ziara yao katika maeneo hayo ya utalii wa kiutamaduni kwa kujionea nyumba za asili za kabila za Wangoni, Wagogo, Wabena, na Wazanaki.

Kila nyumba ya asili iliyokuwa mbele yao walitamani kuingia ili kujionea utunzaji maridhawa wa nyumba hizo.

Kadhalika waliangalia utamaduni wa ngoma za asili ambazo zilijipanga kuwapokea na kuburudika baada ya kutembea.

Kwenye lango kuu la kuingia Kijiji cha Makumbusho kulikuwa na ngoma ya Wadatogo na Wamasai kutoka Ngorongoro wakati na sehemu ya kupumzika kulikuwa na kikundi cha sanaa cha JKT kilichokuwa kimejiandaa kwa ngoma za Kisukuma na Kingoni.

Mrindimo wa ngoma za Kisukuma uliwanyanyua wake hao wa marais na kwenda kucheza na kuwatunza wasanii.

"Hapana muda haujatosha mimi nitarudi kesho kuona vitu hapa," alisema Mke wa Rais wa Commoro, Mama Azali Ambari.

Mama Ambari alisema kuwa vitu viko vingi vya kuona na kuangalia, lakini muda ulikuwa mchache.

Mbali na Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni walitembelea ukumbi wa chimbuko la mwanadamu na kujionea fuvu la mwanadamu wa kale zaidi duniani Zinjanthropus.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya mafuta ya Puma Energy Tanzania, Dominic Dhanah, akizungumza na waandishi wa habari, katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa pongezi kwa Rais Dk. John Pombe Magufuli kwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiswahili sasa rasmi SADC

Na Beatrice Moses

KISWAHILI kimepitishwa kuwa miongoni mwa lugha rasmi zinazotumika kwenye Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Mwenyekiti wa SADC, Rais Dk. John Magufuli, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifunga mkutano wa 39 wa viongozi wakuu wa nchi hizo na serikali.

Alisema Kiswahili kitatumika rasmi katika mawasiliano ya shughuli za SADC, ambayo imekuwa ikitumia lugha tatu ambazo ni Kiingereza, Kireno na Kifaransa.

Katika hatua nyingine aliitaka Sekretarieti ya SADC kutumia fedha za michango kwa manufaa ya wananchi wa nchi wanachama, ikiwamo ujenzi wa zahanati zitakazosaidia kupata huduma za afya hivyo kuokoa maisha yao.

Akizungumzia lugha ya Kiswahili, alisema hatua ya kupitishwa kwa lugha hiyo kuwa rasmi ni faraja kwa Watanzania wote kwa kuwa Hayati Mwalimu Julius Nyerere ndiye aliyeongoza harakati za ukombozi Afrika.

"Mwalimu Nyerere alijitoa kwa moyo alikubali nchi yake ipate shida na watu wake, ili watu wa mataifa mengine wakombolewe," alisema.

Alizitaka nchi nyingine wanancha wa SADC kuiga mfano wa Afrika Kusini wa kuingiza somo la Kiswahili kwenye mfumo wa mafunzo wa elimu kwenye shule zao kuikuza lugha hiyo na kufanikisha utekelezaji wa matumizi yake.

**MATUMIZI FEDHA SADC**


Rais Magufuli aliitaka Sekretarieti ya SADC ambayo inaongozwa na Dk. Stergomena Tax ambaye ni Mtanzania, kuhakikisha fedha za michango zinatumika kwa manufaa ya wana-SADC.

Alisema bajeti ya kuendesha SADC kwa shughuli mbalimbali ikiwamo za maendeleo ni Dola za Marekani milioni 74, kati ya hizo 31 zinatolewa na wafadhili na asilimia 43 zinatokana na wanachama.

"Ni vyema kujitahidi kutumia vyema fedha hizi maana za michango ya nchi za SADC zinatokana na kodi za wananchi wa nchi wanachama, hivyo zilete manufaa," alisema. Alitolea mfano wa matumizi mazuri ya fedha hizo kuwa ni pamoja na kuzipeleka kwenye huduma za afya.

Alisema katika Dola milioni 43 wanaweza kutoa kiasi cha Dola 2,000 na kuzigawanya kwenye ujenzi wa vituo vya afya na kupata vituo 17. Kituo kimoja kinagharimu Sh. milioni 500, kila kituo kinaweza kuhudumia watu 10,000 kwa

INAENDELEA UK. 8



## HABARI KITAIFA

# NGO 158 zaondolewa rejista ya msajili

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MSAJILI wa Mashirika yasiyo ya kiserikali nchini (NGO), Vickness Mayao, ameyaondoa mashirika zaidi ya 158 kwenye rejista ya mashirika yasiyo ya kiserikali.

Mkurugenzi Msaidizi Uratibu wa NGO kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Grace Mbwilo, alitoa taarifa hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi na Msajili wa NGO nchini.

Alisema katika Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya Mwaka 2002, kama ilivyofanyiwa mabadiliko na Sheria Namba 3 ya mwaka 2019, imefafanua kuwa jukumu la kusajili mashirika yanayoendesha shughuli za kijamii, kiutamaduni, kiuchumi, utawala bora, haki za kibinadamu na mazingira katika ngazi ya jamii kwa lengo la kutogawana faida na ambazo hazina mlengo wa kukuza biashara, zimeelekezwa kusajiliwa na Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO).

"Mashirika yaliyoondolewa kwenye Daftari la Msajili wa NGO ni ambayo yalisajiliwa chini ya Sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali Namba 24 ya mwaka 2002 ambayo yanafanya kazi kwa lengo la kunufaisha wanachama wake, kugawana faida, yenye mlengo wa dini na lengo la kukuza biashara na Bodi za Wadhamini," alisema Grace.

Alisema, hatua ya kuyaondoa mashirika hayo kwenye Daftari la Msajili wa NGO imefikiwa kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho Namba 3 ya mwaka 2019, iliyoanza kutekelezwa kuanzia Julai Mosi, 2019. Kwa mujibu wa sheria, mashirika hayo yanatakiwa kwenda kujisajili chini ya sheria husika ikiwamo Sheria ya Jumuiya za Kijamii (Sura ya 337), Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini (Sura ya 318) na Sheria ya Kampuni (Sura ya 212), na kwamba inatakiwa kukamilisha zoezi hilo kabla ya Septemba Mosi, mwaka huu.

Alieleza kuwa kwa kuzingatia ufafanuzi wa mipaka ya usajili ulioainishwa na Sheria Namba

INAENDELEA UK. 8



Mafundi wa ujenzi wakiendelea na kazi ya kumwagia maji kuta za mifereji inayoendelea kujengwa ili saruji ikauke katika eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ripoti: Madereva wazembe wanavyowamaliza Watanzania

**Na Augusta Njoji,** IRINGA

LICHA ya ajali za barabarani kuendelea kupungua, uzembe wa madereva wa magari na pikipiki unatajwa kuchangia zaidi ya nusu ya ajali zote nchini.Takwimu za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani zinaonyesha katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2013 hadi 2017, kiwango cha ajali kimeshuka huku makosa yanayotokana na uzembe wa madereva yakiongoza kwa kusababisha ajali.

Takwimu hizo zinaonyesha madereva wazembe wameendelea kuwa chanzo kikuu cha ajali hizo, zikibainisha kuwa kwa mwaka 2013 pekee, ajali 10,199 kati ya 23,842 zilizotokea, zilitokana na uzembe wao.

Kwa mwaka 2014, ajali 7,320 kati ya 14,360 zilitokana na uzembe wa madereva, huku takwimu za jeshi hilo zikionyesha kuwa kati ya ajali 8,337 zilizotokea mwaka 2015, ajali 3,836 zilitokana na uzembe wa kundi hilo.

Vilevile, kwa mwaka 2016, kati ya ajali 9,856 zilizotokea, 5,391 zilitokana na uzembe wa madereva na mwaka 2017, changamoto hiyo ilisababisha ajali 2,715 kati ya 5,574 zilizotokea.

Jeshi hilo linabainisha kuwa visababishi vingine vikubwa vya ajali za barabarani ni uendeshaji wa hatari, likibainisha kuwa kwa mwaka 2013, kulikuwa na ajali 3,395, mwaka 2014 (1,896), mwaka 2015 (1,041), mwaka 2016 (1,041) na mwaka 2017 (618).

Katika mahojiano na Nipashe mjini Iringa wiki iliyopita, Mkuu wa Kitengo cha Elimu kwa Umma, Makao Makuu ya Kikosi cha

INAENDELEA UK. 8

# Mbaroni kukutwa na dhahabu bandia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashikilia watuhumiwa watatu kwa tuhuma za kukutwa na vipande 10 vya madini bandia aina ya dhahabu wakiwa kwenye harakati za kuyauza wilayani Kahama.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alisema watuhumiwa hao walikuwa na mtambo wa kufyatua madini hayo bandia ya dhahabu ambayo huyauza wilayani Kahama, Geita pamoja na Mwanza.

Alisema katika misako ya uhalifu ambao waliufanya mwezi uliopita mkoani humo, walifanikiwa kukamata watuhumiwa 73 wa matukio mbalimbali ya uhalifu, wakiwamo wezi, wauaji, pamoja na watu watatu wa utengenezaji wa madini bandia ya dhahabu.

"Watuhumiwa hawa tuliwakamata wakiwa na vipande 10 vya madini bandia aina ya dhahabu na walikuwa kwenye harakati za kuyauza wilayani Kahama, na wamekuwa wakiyauza pia Geita, pamoja na Mwanza," alisema Abwao. "Katika msako huo pia tulifanikiwa kukamata watuhumiwa 48 wakihusika na uuzaji madawa ya kulevya aina ya bangi kilo 229, mirungi kilo 117, cocaine kilo 117, heroine gramu 189, pikipiki tatu, Tv sita, Laptop mbili, Sabwoofer moja, pamoja na mitambo ya gongo 27," aliongeza.

Alisema pia walifanikiwa kukamata watuhumiwa wanne waliohusika na matukio ya mauaji ya Kalekwa Shiku (50) mkazi wa kijiji cha Mishepo, Shinyanga vijijini, ambaye aliuawa kwa kufunikwa mfuko usoni, kufungwa mawe miguuni, na kisha kuzamishwa kwenye bwala la maji na kufariki dunia.

Alisema watuhumiwa hao walitekeleza mauaji hayo Juni 6, mwaka huu, kwa madai ya tamaa ya kutaka kujipatia ng'ombe tisa kwa mwanamke huyo na baada ya kugoma ndipo waKatekeleza mauaji hayo.

Alisema watuhumiwa wote waliohusika na matukio hayo ya uhalifu na mauaji mkoani humo, wanawashikilia na upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani ili sheria ifuate mkondo wake.


## BONITE BOTTLERS LIMITED

### Advertisements of Employment

### 1. Mechanical Technician

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of Bachelor Degree /Diploma in Mechanical Engineering from a recognised Institution.

**Key skills & Abilities:**

- Ability to maintain all the mechanical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the Line and service equipment by close communication with other staff.
- Ability to operate the machines as directed and to ensure they are running smoothly and efficiently as required and kept clean as required.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated and flexible person and a good team player

### 2. Electrical Technician

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of Bachelor Degree/Diploma in Electrical Engineering from a recognized institution.

**Key skills & Abilities:**

- Ability to maintain all the electrical equipment to acceptable and approved standards for efficient operation, and to ensure the smooth running of the Line and Service equipment by close communication with other staff
- Ability to operate the machines as directed and to ensure they are running smoothly and efficiently as required and kept clean as required.
- Ability to ensure the correct electrical functioning of all electrically operated machines on the premises.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated and flexible person and a good team player

- **Experience:** 4 years or above in Mechanical/Electrical field.
- **Deadline date :** 21.08.2019
- **Location:** Moshi.

**Mode of Application:**

All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned address to reach him not later than 21/08/2019.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352, MOSHI**

615378002

## HABARI KITAIFA



Meneja wa Vodacom Tanzania Plc Wilaya ya Kinondoni, Suleiman Amri, akimsajili Mama Maria Nyerere kwa njia ya alama za vidole nyumbani kwake jijini Dar es Salaam. Kampuni hiyo inaendelea kuunga mkono zoezi hilo lililobainishwa na serikali na kuhamasisha watu wote kujisajili kwa njia ya alama za vidole ambayo ni ya haraka na haina gharama yoyote. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lori mafuta lateketea, laua, kujeruhi dereva

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

LORI mali ya Kampuni ya Mount Meru lililokuwa limebeba shehena ya mafuta, limeanguka na kuwaka moto papo hapo katika Kijiji cha Shunu Kata ya Nyanganga, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga na kusababisha kifo cha mtu moja na kujeruhi dereva.

Aliyefariki dunia ametajwa kuwa ni utingo aliyefahamika kwa jina moja la Erick (22) na kumjeruhi dereva, Ibrahimu Issa.

Lori hilo lenye namba za usajili RAD 416V na tela namba RL 1950 lilianguka usiku wa kuamkia Jumamosi likitokea jijini Dar es Salaam kuelekea Rwanda, lilianguka na kuwaka moto wakati likikwepa gari dogo aina ya Toyota Voltz.

Kube Shija, Mwenyekiti wa Kijiji cha Shunu, alisema kuwa walisikia mlipuko wa moto majira ya saa saba usiku na walipofika katika eneo hilo walikuta lori hilo likiwa linateketea kwa moto, huku mwili wa dereva uliwaka moto.

Alisema baada ya kuona tukio hilo walitoa taarifa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili waje kuzima moto huo, na walifanikiwa kumwokoa dereva na kumkimbiza katika Hospitali ya Mji wa Kahama kupatiwa matibabu.

"Tulisikia mlipuko mkubwa sana usiku wa saa saba, na tulifika eneo hilo tulikuta lori la mafuta likiwa linawaka moto, na tulifanikiwa kumwokoa dereva wa gari ambae tulimkuta akiwa anagalagala chini

INAENDELEA UK. 26

# Serikali yaagiza kampuni kulipa ushuru mgodini

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

KAMPUNI tanzu mkoani Geita zinazofanya kazi ya kutoa huduma katika kampuni ya uchimbaji madini ya Geita Gold Mining (GGM) zimetakiwa kulipa ushuru wa huduma (service Levy) kwenye halmashauri husika mkoani Geita.

Serikali imesema kwa kufanya hivyo, serikali itapata mapato yake. Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhandisi Robert Gabriel Luhumbi, wakati wa hafla ya kutiliana saini hati ya makubaliano ya fedha ya uwajibikaji kwa jamii CSR kwa mpango kazi wa mwaka 2019/2020 kati ya Halmashauri mbili za Mji na Halmashauri ya Geita na GGM.

Gabriel alisema kuna baadhi ya kampuni tanzu zinazofanya kazi ya kutoa huduma kwenye mgodi wa GGM zinakwepa kulipa ushuru wa huduma kwenye halmashauri na kusababisha halmashauri kukosa mapato stahiki na hivyo kuzitaka kampuni hizo kuanza kulipa haraka ushuru huo.

"Kuna baadhi ya kampuni tanzu zinafanya kazi ya kutoa huduma kwenye mgodi wa GGM, lakini zinakwepa kulipa ushuru wa huduma kwenye Halmashauri za Mkoa wa Geita. Kampuni hizo nazitaka zianze kulipa mara moja," alisema.

Utilianaji saini ya hati ya makubaliano hayo baini ya halmashauri hizo na GGM ulipokelewa kwa shangwe na viongozi wa vyama vya siasa, dini na watendaji wa serikali baada ya Halmashauri ya Mji Geita kutajwa kuwa imekuwa ya kwanza kitaifa kwa kukusanya mapato ambapo halmashauri ya Geita nayo imeingia katika halmashauri tano bora katika ukusanyaji wa mapato nchini.

Gabriel alisema halmashauri hizo zimeuletea heshima kubwa Mkoa wa

INAENDELEA UK. 26

# Tanzania yapigiwa debe kwa uwekezaji

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa China nchini, Wang Ke, amesema Tanzania ni sehemu nzuri ya uwekezaji kutokana na kuwa na soko la uhakika, nguvukazi na bandari, hivyo anategemea wawekezaji zaidi mwaka huu kutoka nchini humo kuja kuwekeza.

Ke alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa msaada wa samani za ofisi kwa ajili ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zanye thamani ya Sh. milioni 45 kuhakikisha kituo hicho kinahudumia vema wawekezaji.

Balozi huyo alisema anategemea mwaka huu wawekezaji wengine kutoka China kuja Tanzania kutokana na serikali ya Rais John Magufuli kuboresha mazingira.

"Sera mbalimbali zimekuwa zikifanyiwa kazi lakini mwaka huu kumekuwa na kuondoa kodi na tozo mbalimbali zilizokuwa kero kwa wawekezaji hivyo kuongeza mazingira bora kwa wawekezaji Tanzania," alisema.

Alisema China inaongoza kwa uwekezaji nchini na kwamba anaamini wawekezaji wengi zaidi wataongezeka Tanzania hususan baada ya kukamilika kwa mpango wa ufanyaji biashara 'Blue Print'.

Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe, alishukuru kwa msaada huo ambao alisema utasaidia katika ofisi zao mpya hususan za Dodoma.

Alitaja baadhi ya samani walizopokea ni viti, meza na kabati kwa ajili ya ofisi mpya watakayoamia hivi karibuni.

Alisema TIC wana mradi Dodoma wa ujenzi wa ofisi ili kuwa karibu na serikali.

Alisema katika matumizi ya malighafi zilizopo nchini wamekuwa wakitengeneza samani Magereza na tayari walitoa oda, lakini walizopokea zimenunuliwa katika maduka ya samani kutokana na sababu mbalimbali.

TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
ISO 9001: 2015 CERTIFIED
MKUTANO WA 39 WA SADC




Hongera Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwa Mwenyekiti wa SADC. Tunakupongeza sana!
tratanzania
"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ufungiaji viwanja Ligi Kuu uwe endelevu

**JUMAMOSI** wiki hii Ligi Kuu Bara msimu wa 2019/20, utaanza rasmi baada ya mwishoni mwa wiki Simba na Azam kucheza mechi ya Ngao ya Jamii ambayo ni maalum kwa ajili ya kuashiria kuanza kwa msimu mpya.

Ligi hiyo ambayo awali ilikuwa ianze Agosti 23, mwaka huu kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba kukutana na JKT Tanzania, itaanza rasmi Agosti 25 kutokana na mchezo huo wa ufunguzi kusogezwa mbele kufuatia Wekundu wa Msimbazi hao kukabiliwa na mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Jumapili dhidi ya UD Songo ya Msumbiji katika Uwanja wa Taifa.

Hata hivyo, kuelekea ligi hiyo ambayo kama ilivyokuwa msimu uliopita, itashirikisha tena timu 20, kwa mtindo wa kucheza nyumbani na ugenini, na mwisho wa msimu bingwa atakayepatikana atabeba jukumu la kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, ligi hiyo imekuwa ikiandamwa na changamoto kubwa ya ubovu wa viwanja vinavyotumika na tayari Bodi ya Ligi kupitia Mkurugenzi Mtendaji wake, Boniface Wambura wiki iliyopita ilitangaza uamuzi uliofikiwa wa kuvifungia baadhi ya viwanja kutokana na kutokidhi vigezo vya kuchezwa ligi hiyo.

Viwanja vilivyofungiwa hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho na bodi hiyo kujiridhisha, ni Uwanja wa Mwadui Complex (Shinyanga), Manungu (Morogoro) na Mabatini (Pwani).

Kufungiwa kwa viwanja hivyo, itabidi Mtibwa Sugar inayotumia Uwanja wa Manungu kwa mechi zake za nyumbani, Ruvu Shooting (Mabatini) na Mwadui FC (Mwadui Complex) kutafuta viwanja vingine kwa ajili ya mechi zao za nyumbani hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho.

Kwa ujumla ukiondoa Uwanja wa Taifa na Uhuru ambavyo hutumiwa na timu za jijini Dar es Salaam na ule wa Azam Complex, Chamazi (Azam FC), Kaitaba (Kagera Sugar), CCM Kirumba (Mbao FC) na Nyamagana (Alliance FC), kwa asilimia kubwa vilivyosalia si rafiki kwa timu kuweza kucheza soka la kuvutia lakini Bodi ya Ligi imemulika upande mmoja tu wa usamala kwa mashabiki na kuachilia mbali ubora wa eneo la kuchezea (pitch).


Tunatambua moja ya mambo ambayo yanakwamisha soka letu kuweza kupiga hatua mbele ni pamoja na miondombinu mibovu ya viwanja, hivyo kuna haja ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kupitia Bodi ya Ligi Kuu, kutosita kuendelea kukagua eneo la kuchezea na kuvifungia viwanja vibovu.

Hatuoni sababu kwa Bodi ya Ligi Kuu kuendelea kufumbia macho viwanja vingine ambavyo eneo la kuchezea kutokuwa rafiki kwa wachezaji hasa ukizingatia klabu huingia gharama kubwa kuwatibu wachezaji wao wanapoumia.

Matarajio yetu ni kuona viwanja ambavyo Bodi ya Ligi Kuu imejiridhisha kwamba vinakidhi vigezo, vikiendelea kuhudumiwa kwa msimu mzima na ukaguzi ukifanyika mara kwa mara na pindi vitakapobainika kutokidhi vigezo hatua ya kuvifungia ichukuliwe mara moja na si kama ambavyo Bodi ya Ligi imevifungia viwanja hivyo kwa sababu tu eti havina uzio unaotenganisha eneo la kuchezea na mashabiki, vilivyo na uzio ni wa mabati ama makuti. Watanzania wanapenda sana soka, lakini moja kati ya mambo yanayowanyima uhondo wa kufurahia burudani hiyo, kubwa ni ubovu wa viwanja hususan eneo la kuchezea, suala ambalo kama Bodi ya Ligi Kuu itaendelea kulimulika mara kwa mara na kutoa adhabu ya kuvifungia vilivyo vibovu, hakika linaweza kumalizika.

Tunaamini suala la kuvikarabati, linawezekana hasa kutokana na kiasi kikubwa cha mapato ambacho wamiliki hukipata kutokana na viwanja hivyo kutumika na timu husika, hivyo pasipo msukumo mkubwa wa ukarabati, klabu, TFF na serikali kwa ujumla zitaendelea kupoteza mapato kutokana na watazamaji kutoshawishika kwenda uwanjani, huku Watanzania wakikosa burudani waliyotarajia. Nipashe tunakiri kufurahishwa na hatua iliyochukuliwa na Bodi ya Ligi Kuu kuvifungia baadhi ya viwanja vibovu, lakini tunatamani kuona zoezi hilo likiwa endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi sawa waadhibiwe, lakini walipwe kwa wakati

Na Adam Fungamwango

**KABLA** msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa 2019/20 haujaanza, tayari waamuzi watakaochezesha wamepigwa mkwara kuwa yeyote atakayeonekana kuchezesha vibaya, au kwenda kinyume na sheria za soka, basi ataondolewa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi, Salum Chama, amesema kuwa wameweka sheria kali ya kuwabana waamuzi kwa msimu ujao, ambapo watakuwa wanafuatilia kuanzia mechi ya kwanza na atakayebainika kwenda kinyume watamwondoa haraka.

"Hatutamvumilia mwamuzi atakayekwenda kinyume cha kanuni, yapo makosa ya kibinadamu yanaweza kutokea, lakini tukibaini mwamuzi amepindisha sheria, huku akifahamu, tutamfuta moja kwa moja," anasema na kuongeza.

"Mfano kuna mambo ya kukataa bao ambalo ni halali, au kutoa kadi kwa mchezaji asiyestahili, kwa kweli mwamuzi kama huyo mara moja tutaanza naye, lengo ni kuboresha sekta hii," anasema.

Hili ni jambo ambalo litawafanya sasa waamuzi wawe makini wanapokuwa wanachezesha soka, lakini pia watakuwa wakitoa maamuzi sahihi na kuachana na maamuzi tata ambayo mashabiki wengi wanakuwa na tafsiri kuwa amechukua rushwa, au ana mapenzi na timu fulani.

Ukweli ni kwamba klabu zinajiandaa kukaa kambini, zinaingia gharama kubwa kuwa na wachezaji bora, kuwalipa vizuri, lakini mwamuzi mmoja anaingia na matokeo yake mfukoni, akitaka kufanya kila hila ili timu yenye uwezo isiibuke na ushindi.

Hapo ndipo huwa tunaona vituko baada ya vituko. Lakini pia Chama aangalie upande wa pili kama waamuzi hao wanalipwa stahiki zao vema, ili kutoingia kwenye ushawishi wa kupanga matokeo.

Kuna taarifa kuwa waamuzi wengi wamekuwa wanacheleweshewa stahiki zao. Vile vile inaelezwa kuwa waamuzi wengi huwa wanakwenda kuchezesha vituoni wakitumia nauli zao na kukaa hotelini kwa gharama zao na wanafanya hivyo hadi pale watakapokuja kulipwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF). Hali kama hii inakaribisha kabisa harufu ya rushwa kwani kama timu mwenyeji ikiamua kumgharamia mwamuzi au waamuzi hao hoteli na chakula tu, achilia mbali pesa ya mfukoni, basi anaweza kuwakirimu kwa kuwachezesha kwa upendeleo.

Mimi nadhani kabla ya mkwara huu, Chama angewaambia waamuzi wote kuwa kuanzia sasa watalipwa kwa wakati posho zao, hivyo hakuna kisingizio chochote, atakayevurunda cha moto atakiona.

Sina maana kuwa kwa sababu mwamuzi anacheleweshewa stahiki zake, basi ndiyo afanye madudu, lakini hii itamfanya asiwe na kisingizio kuwa labda alikuwa na msongo wa mawazo kutokana na kutokuwa na pesa mfukoni.

Waswahili wanasema haki na wajibu, waamuzi wanaweza kuwa na visingizio tele kama wataendelea kukopwa na wanaweza kuwa na watetezi, lakini kama wakilipwa vizuri na kwa wakati sidhani kama kutakuwa na mtu anayeweza kuwa na huruma nao kama wakivurunda mechi yoyote ile.

Lakini pia waamuzi hawa wasiwe wanafungiwa au kuondolewa kwenye ligi kwa shinikizo la mitandao ya kijamii. Kumezuka tabia ya mihemko ya mashabiki hasa wa timu kubwa kushinikiza waamuzi wapewe adhabu hata kama kosa lenyewe ni la bahati mbaya au la kibinadamu.

Na waamuzi wanaopata matatizo hayo mara nyingi huwa ni wale wanaochezesha timu kubwa za Simba, Yanga na Azam. Cha ajabu kuna baadhi ya malalamiko kutoka kwenye timu zingine, lakini kwa sababu ni mechi ambazo hazizihusu klabu hizo kubwa, basi waamuzi hawachukuliwi hatua yoyote.

Mwenyekiti huyo pia anapaswa aziangalie zaidi mechi ambazo hazionyeshwi laivu kwenye televisheni. Uchunguzi wangu mdogo tu unaonyesha kuwa baadhi ya mechi chache ambazo hazionyeshwi zinakuwa na matokeo yenye utata mkubwa na malalamiko kuwa waamuzi wanafanya chochote wanachojisikia kwa sababu hawaonekani.

Mechi kama hizi hata kama hazionyeshwi, zinapaswa ziangaliwe kwa jicho la tatu kwa kutuma waangalizi ambao watapeleka taarifa moja kwa moja kwenye kamati hiyo. Yangu ni hayo tu katika hilo.

## Wavuta sigara wafuate sheria

**Mhariri**

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyo nayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*

*Tabia hii kimsingi inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

**Joseph Zengo-Malampaka, Simiyu**

## Tusifumbie macho uhalifu huu

**Mhariri,**

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utapata jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinavyosisitiza juu ya hilo.*

*Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo majalalani ama kwenye vyoo wakati mwingine na hivyo kukatisha maisha ya watoto wasio na hatia.*

*Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari.*

*Ninawatahadharisha watu wanaofanya unyama huo wakumbuke kwamba Mwenyezi Mungu anawaona. Ninaomba kwa serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

**Imran Komba, Songea**

**WASILIANA NASI:**
TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# TFF inapokula samaki upande mmoja ufungiaji wa viwanja



Mkurugenzi wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura.

**Na Adam Fungamwango**

**SHIRIKISHO** la Soka nchini (TFF) kupitia Bodi ya Ligi, limevifungia viwanja vitatu maarufu nchini visitumike kwenye Ligi Kuu hadi hapo vitakapofanyiwa marekebisho.

Viwanja hivyo ni Mwadui Complex kilichopo Shinyanga, Manungu Complex kilichopo Turiani mkoani Morogoro na Mabatini kilichopo Mlandizi mkoani Pwani.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi, Boniface Wambura, anasema kuwa wameamua kuvifungia kutokana na kubainika kuwa uzio wa viwanja hivyo ni hatari kwa mashabiki na wachezaji wenyewe kwani baadhi vimezungushiwa mabati na vingine makuti.

Wambura anasema kuwa ukaguzi wa viwanja bado unaendelea na hawatosita kukifungia kiwanja chochote ambacho hakitokidhi matakwa.

Kutokana na hali hiyo, timu ya Mwadui ambayo inatumia Uwanja wa Mwadui Complex sasa italazimika kucheza mechi zake za nyumbani kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga, Ruvu Shooting inayotumia Uwanja wa Mabatini kama uwanja wake wa nyumbani, itatumia Uwanja wa Meja Isamuhyo ambao pia hutumiwa na JKT Tanzania kama uwanja wa nyumbani.

Timu ya Mtibwa Sugar ambayo hutumia Uwanja wa Manungu, italazimika kuwa Uwanja wa Jamhuri Morogoro ikizisubiri timu zingine.

Viwanja hivyo vitatu vimebainika kuwa vimezungushiwa mabati, na pia kuna maeneo ambayo yamezungushiwa makuti.

Kwanza kabisa ni kwamba Bodi ya Ligi ilichelewa kupiga marufuku viwanja hivi. Ni hatari sana kucheza kwenye viwanja ambavyo vimezungushiwa mabati na makuti kwa sababu vitu hivyo vinaweza pia kuwa silaha kwa mashabiki wakorofi viwanjani.

Mashabiki wa soka wanatoka sehemu mbalimbali na ni watu wenye tabia mbalimbali, wengine hasira zao ziko karibu, akitaniwa tu na mwenzake, basi anapandwa na jazba, hivyo kipande cha bati, au makuti ambayo katikati huwa na mti mwembamba, inaweza kuwa silaha.

Pia kuna mashabiki wenye jazba kwa wachezaji wao au pinzani, wanaweza kabisa kutumia vitu kama hivyo kuwadhuru.

Itakuwa haina maana kama mashabiki wanakatazwa kuingia uwanjani na chupa za maji, au silaha ya aina yoyote, lakini kumbe uzio tu wa uwanja wenyewe ni silaha tosha.

Kwa hili, Bodi ya Ligi inabidi ipongezwe. Hata hivyo bado imeonyesha mapungufu baadhi ya maeneo. Nilitegemea viwanja zaidi ya vitatu kufungiwa na si hivi ambavyo vina matatizo ya uzio.

Kuna viwanja ambavyo vina matatizo ya vyoo na sehemu za kuchezea. Tuliona msimu uliopita Ligi Kuu ikichezwa kwenye viwanja vibovu.

Baadhi ya viwanja sehemu ya kuchezea ni kavu kana kwamba nchi hii haijaonyesha mvua mwaka mzima, au kiwanja kiko sehemu za Jangwani, lakini kuna viwanja ambavyo ni karibu uwanja mzima hakuna majani, vikiongozwa na Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

Vipo viwanja vyenye majani, lakini ni kama vina matuta-matuta, mpira ukichezwa unakuwa unadunda bila mpangilio.

Kusema kweli viwanja hivi si tu kwamba vinawanyima raha mashabiki kuangalia kandanda lenye burudani badala yake wanashuhudia butua-butua, lakini pia vinawafanya wachezaji kuonyesha vipaji vyao halisi na badala yake kucheza kutokana na matakwa ya uwanja ulivyo.

Achilia mbali hayo, viwanja hivyo havileti hata mwonekano mzuri kwenye televisheni ambazo zinaonyesaha Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa kawaida, viwanja vinavyokuwa bora hasa sehemu ya kuchezea, humvutia hata mtazamaji kutokana na rangi nzuri ya kijani inayoonekana uwanjani, tofauti na hapo inakuwa ni karaha tu kwani macho wanachoona ni vumbi, au udongo mkavu.

Nadhani imefika wakati sasa Bodi ya Ligi kuangalia pia suala la sehemu ya kuchezea uwanjani na si uzio peke yake ili kupata ligi bora, yenye ushindani, baadhi ya timu zikiwa na uwezo wa kwenda kucheza mfumo wowote kwenye uwanja, vile vile kupunguza mlalamiko na visingizio vya baadhi ya makocha 'tumefungwa kwa sababu uwanja mbovu'.

Natumai kuona hili nalo likiangaliwa kwa mustakabali wa maendeleo ya soka la Tanzania kwani kwa muda mrefu sasa, sehemu ya kuchezea mpira kwenye viwanja vingi nchini, ukiondoa Uwanja wa Taifa, Chamazi, Uhuru, Kaitaba, CCM Kirumba na Nyamagana ni majanga matupu.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUKANUSHA HABARI YA KUTANGAZA NAFASI ZA KAZI 500 KWA VIJANA WA TANZANIA**

**Dar es Salaam, 18 Agosti, 2019.**

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa inayosambaa katika mitandao ya kijamii yenye kichwa cha habari ***"Mamlaka ya Mapato Tanzania (Tanzania Revenue Authority) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha pamoja na Benki Kuu ( BOT)"***.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), inatangaza nafasi za kazi 500 za uelimishaji wa namna ya uchangiaji kodi pamoja na ukusanyaji wa Kodi ya Majengo vijijini.

TRA inakanusha taarifa hiyo na inauomba Umma kuipuuza kwa sababu haina ukweli wowote na ifahamike kuwa, mawasiliano yaliyopo kwenye taarifa hiyo sio mawasiliano rasmi ya TRA.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali piga simu bure Kituo cha Huduma kwa Wateja kupitia namba **0800 750 075** au **0800 780 078** au tuma barua pepe: **huduma@tra.go.tz**, au tembelea tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania: **www.tra.go.tz**. Pia, unaweza kutuma ujumbe kwa njia ya WhatsApp kwenda namba **0744-233-333**.

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Imetolewa na;
**Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi,
TRA MAKAO MAKUU.**

## Wakuu SADC watoka na maazimio mazito

INATOKA UK. 2

kitasaidia nchi wanachama kukabiliana na majanga kama vile mafuriko, ukame, njaa, magonjwa ya mlipuko.

**VIKWAZO UCHUMI**

"Wakuu pia walipitia hali ya uchumi katika ukanda wetu, nchi za SADC zimetakiwa kuwekeza katika miundombinu kwa kuwa ndiyo kikwazo kikubwa cha ukuaji uchumi kwenye Bara la Afrika ikiwamo SADC," alisema Rais Magufuli.

Pia walikubaliana kuboresha sera za uchumi na fedha, ili kuboresha mazingira ya ukuaji uchumi katika ukanda wa SADC.

**BURUNDI KUJIUNGA SADC**

Alisema pia walijadili suala la upatikanaji wa mapato, pamoja na Burundi kujiunga na SADC na kwamba wakuu hao wameielekeza Burundi kukamilisha baadhi ya maeneo, kisha kamati ya SADC itakwenda kuangalia ndipo maamuzi yatolewe.

**VIKWAZO ZIMBABWE**

Alisema kuhusu Zimbabwe, wakuu hao wamekubaliana kuendelea kufanya mawasiliano na jumuiya za kimataifa ili kuwezesha kuondolewa kwa vikwazo kwa nchi hiyo, kupitia balozi na jumuiya mbalimbali.

"Kwa kauli moja tumetamka kuwa tupo pamoja na Zimbabwe na hatutaiacha," alisema Rais Magufuli.

Kuhusu suala la mapato, Rais Magufuli alisema wakuu hao walizipongeza nchi zilizokamilisha katika kutoa michango na ada zao kwa mwaka, na kuzihimiza zingine ambazo hazijatoa kutimiza wajibu wao.

## Ripoti: Madereva wazembe

INATOKA UK. 4

Usalama Barabarani, Abel Swai, alisema uzembe na uendeshaji wa hatari kwa madereva ni miongoni mwa makosa ya kibinadamu yanayochangia kwa kiwango kikubwa ajali za barabarani licha ya Jeshi la Polisi kuweka mikakati ya kudhibiti hali hiyo.

Alisema jeshi hilo limekuwa likitoa elimu kwa madereva, kuendesha ukaguzi na kubaini baadhi ya madereva wanaosababisha ajali hizo kunatokana na kuendesha bila kupewa mafunzo.

Alisema katika ukaguzi wao hao, wamekuwa wakibaini baadhi ya madereva wana leseni lakini wamezipata kwa njia zisizo rasmi.

"Kulikuwa na malalamiko mengi kuhusu utoaji wa leseni kwamba zinatolewa ovyo. Ni kweli awali ilikuwa hali hiyo lakini hivi sasa tumedhibiti.

"Jambo tunalotakiwa kuachana nalo Watanzania ni suala la kukwepakwepa, tuache, ni hatari. Sasa hivi tunashirikiana vizuri kabisa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwenye utoaji wa leseni," alisema.

Aliongeza kuwa kwa sasa kuna ukaguzi unaendelea wa shule za udereva katika Jiji la Dar es Salaam na wamebaini baadhi ya wakufunzi wa shule hizo hawajakidhi vigezo kwenye utoaji wa mafunzo ya udereva na kulazimisha kuwarudisha shuleni.

"Hawa wakufunzi wanasoma na tutaenda kwenye mikoa mingine, tuhakikishe kweli wanayofundishwa kwa madereva ni yale yanayotakiwa ili tuondokane na ajali zinazotokana na uzembe na uendeshaji wa hatari wa kutotii sheria za barabarani," alisema.

Swai alibainisha kuwa kuna aina tatu za mitihani inayotolewa kwa madereva, mmoja ukitungwa na chuo husika huku miwili ikitungwa na Jeshi la Polisi.

"Tuna mitihani mitatu kwa ajili ya madereva, kwa upande wetu Jeshi la Polisi ipo mitihani miwili upo wa kuandika ambao una maswali 50 na ukifaulu unaenda kufanya mtihani wa vitendo.

"Ukifeli unatakiwa kurudi darasani mpaka uelewe, sasa baada ya mchakato huu, polisi tunajaza taarifa za mhusika kwenye mtandao ambazo zinakwenda moja kwa moja TRA kwa ajili ya michakato mingine ya kupata leseni," alisema.

Swai pia alisema kampeni ya 'nyakua kimyakimya' inaendelea ili kudhibiti uzembe kwa madereva kwa kukamata na kuchukua hatua kali dhidi ya madereva wanaobainika kuendesha bila kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Wakati jeshi hilo likiendelea kuchukua hatua hizo, Jumamosi ya wiki juzi, katika eneo la Msamvu Itigi mkoani Morogoro, lori la mafuta lilianguka wakati dereva wake akijaribu kumkwepa mwendesha pikipiki (bodaboda).

Ajali hiyo baadaye ilisababisha vifo vya watu zaidi ya 90 baada ya tangi la mafuta la lori hilo, kulipuka wakati baadhi yao wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.




## NGO 158 zaondolewa rejista ya msajili

INATOKA UK. 4

3 ya mwaka 2019, Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), anayakumbusha mashirika yanaofanya shughuli kwa lengo la kugawana faida, yenye mlengo wa dini na ambayo yana malengo wa kukuza biashara, kwamba mashirika ya aina hiyo yatafutwa kwenye Daftari la Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali baada ya kipindi cha miezi miwili kuanzia Julai Mosi, 2019 na yatahamishiwa chini ya mamlaka nyingine za usajili kutokana na kukosa sifa ya kuwa NGO.

Katika kuhitimisha usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali uliofanyika mkoani Mbeya, Ofisi ya Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali imewaagiza wadau wa mashirika yote yaliyosajiliwa kwa lengo la kuzalisha faida na kugawana faida kuhakikisha kuwa wanahamisha usajili ili kuhuisha taarifa zao kwa Msajili stahiki.

Hatua hiyo imechukuliwa na Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika hatua ya mwisho ya usajili wa mashirika hayo kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayohitimishwa mwisho wa wiki jijini Mbeya na orodha ya mashirika 158 yaliyoondolewa kwenye daftari inapatikana katika tovuti ya wizara www.mcdgc.go.tz na ya mashirika yasiyo ya kiserikali. www.tnnc.go.tz

## Kiswahili sasa rasmi SADC

INATOKA UK. 3

mwaka.

Alisema pia SADC wamejiweka mpango wa kujiongezea mapato kwa namna ambayo nchi wanachama itaona ni njia bora ya kuchangia michango waliyokubaliana.

Mwenyekiti huyo wa SADC alisema wamekubaliana na wakuu wengine wa nchi hizo kuziaomba jumuiya za kimataifa kuondoa vikwazo ilivyoweka kwa nchi ya Zimbabwe.

Wakati huo huo, alisema kuwa maombi ya nchi ya Burundi kujiunga na SADC yanafanyiwa kazi, kwa kuwa kuna mambo ambayo nchi hiyo bado haijakamilisha.

Awali, akihutubia baada ya kukabidhiwa nafasi hiyo juzi aliitaka sekretarieti hiyo kujitathimini na akibainisha kuwa imeshindwa kutoa majibu ya kwa nini uchumi wa nchi wanachama haujafikia malengo ya kukuza uchumi kama walivyokubaliana.

Alisema inasikitisha kuona nchi za Afrika zikiwamo za SADC kuendelea kujiita maskini wakati zina ardhi, madini, rasilimali watu, nishati na misitu ya kila aina.

Rais Magufuli ambaye alipokea uenyekiti kutoka kwa Rais wa Namibia Hage Geingob, alisema katika kikao cha marais walichokutana kwa pamoja wamempongeza mwenyekiti aliyemaliza muda wake kwa kazi kubwa aliyofanya.

Nchi za SADC zinazotajwa kuwa na watu zaidi ya milioni 370 na ukubwa wa heka zaidi ya milioni 9.8, miongoni mwa nchi hizo 10 zipo kwenye orodha ya nchi maskini duniani.

Mwenyekiti huyo alisema kwa uchunguzi wake amebaini kitendo cha nchi za SADC kuagiza vyakula kutoka nje ni kutokana na kukosekana kwa taarifa, hivyo kuna mahali hawapo sawa katika kutoa taarifa.

Alieleza kusikitishwa kwake na mtazamo ulio miongoni mwao hasa kuamini bidhaa ikiwamo, chakula bora ni kutoka nje ya SADC, licha ya kwamba miongoni mwa nchi wanachama zinazalisha mazao mengi.

Dk. Magufuli alisema changamoto nyingine ambayo ameibani kukwamisha maendeleo na kukua kwa uchumi kwa nchi wanachama ni kutokana na kuwapo kwa sheria, sera na kanuni ambazo haziwiani hivyo kukwamisha biashara.

Aliahidi kuwa chini ya uenyekiti wake suala la viwanda litakuwa kipaumbele chake cha kwanza, ingawa mambo yote yanaweza kufanikiwa kama rushwa itadhibitiwa.

Rais wa Msumbiji Filipe Nyusi, Makamu Mwenyekiti wa SADC, alisema kama Rais wa Msumbiji atashirikiana na Rais Magufuli katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wao na kuhakikisha kasi anayoitaka wanakwenda nayo.

Nyusi alisema pia wanajiandaa kupokea Mkutano wa 40 wa SADC ambao unatarajiwa kufanyika Msumbiji mwezi Agosti mwakani.

"Napenda kukuhakikishia kuwa tumejipanga kwenda na kasi yako, ili tuweze kutekeleza malengo tuliyojiwekea SADC," alisema.

Mkutano huo ulimchagua Rais Emerson Mnangagwa wa Zimbabwe kuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Siasa, Ulinzi na Usalama (SADC Troika).

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, mwishoni mwa wiki, kuhusu walivyojipanga kukabiliana na viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki na baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiingiza na kusambaza mifuko hiyo kwa njia za magendo. Kulia ni Mkurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Yusuf Ngenya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasabato wahamasishwa kujiandikisha kupiga kura

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAUMINI wa Kanisa la Waandiventista Wasabato Shinyanga Mjini, wametakiwa kwenda kujindikisha kwenye daftari la kudumu la mpigakura, ili waweze kupiga kura kwenye chaguzi ujao ukiwamo uchaguzi mkuu mwakani, na kuwachagua viongozi ambao watawaletea maendeleo.

Uandikishaji wa daftari la kudumu la mpiga kura linatarajiwa kuanza mkoani Shinyanga Agosti 26 hadi Septemba Mosi mwaka huu, ambapo watakaohusika kuandikishwa ni wale ambao walishapoteza kadi zao za kupigia kura, ambao zimeharibika, ambao hawajawahi kujiandikisha na watakaokuwa wameshafikisha umri wa miaka 18.

Rai hiyo ilitolewa juzi kanisani na Mchungaji wa Kanisa la Waandiventista Wasabato Shinyanga Mjini, John Kilinda, wakati akitoa matangazo ya kanisa kwa waumini wa kanisa hilo.

Alisema waumini wote wa kanisa hilo ambao wana sifa ya kupiga kura ni wenye umri wa kuanzia miaka 18 na wale ambao mwakani watakuwa na umri huo, pamoja na waliopoteza kadi zao za kupigia kura waende kujiandikisha pale zoezi litakapo anza, huku akitoa tahadhari kutojiandikisha mara mbili kuwa ni kosa la jinai.

"Mimi sina itikadi yoyote ya kisiasa, najua kuna waumini humu kila mmoja ana itikadi yake yupo chama fulani, lakini nachokisema hapa ni kuhamasisha tu, wale wenye kufikisha umri wa miaka 18, na mliopoteza kadi zenu za kupigia kura, zoezi litakapo anza muende mkajiandikishe kwenye daftari la kudumu la mpigakura," alisema Kilinda.

"Hivi karibuni wadau wa uchaguzi tukiwamo viongozi wa dini, tulikuwa na kikao na Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Balozi Omari Ramadhani Mapuri, akituhamasisha tutoe hamasa kwa waumini wetu wajitokeze kwa wingi kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la mpigakura, ndio maana nimetoa hamasa," aliongeza.

Aidha, mwishoni mwa wiki iliyopita Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikiongozwa na Mapuri, walifanya kikao na wadau wa uchaguzi mkoani Shinyanga, wakiwamo wana siasa, asasi za kiraia, wanahabari, na viongozi wa dini, ambacho lengo ni uhamasishaji wananchi wajitokeze kujiandisha kupiga kura.

Mapuri alisema wadau hao ni wa muhimu kwenda kutoa hamasa kwa wananchi ili wajitokeze kwa wingi kwenda kujiandikisha kwenye daftari la kudumu la mpigakura.

# NMB yaiahidi ushirikiano serikali

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa Benki ya NMB kutokana na jitihada zake za uboreshaji wa huduma za kijamii na kukuza uchumi wa wananchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya Siku ya Nyumba ya Benki ya NMB mwishoni mwa wiki jijini Mbeya, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema Benki ya NMB imeisaidia serikali kuboresha hali za wananchi wake.

"Tumekuwa tukiiona NMB ikipandisha watu kiuchumi, tunawaomba sera zenu zisimamiwe vizuri ili wananchi wengi wanufaike na mikopo inayotolewa na Benki yenu," alisema Chalamila.

Aidha, ameishauri Benki ya NMB kuelekeza zaidi elimu ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wamachinga wanaotarajiwa kukua na kuwa wakopaji wakubwa baada ya kuongezeka mitaji yao. "Ningependa kuona biashara za hawa wamachinga na wajasiriamali wadogo zikikua, ili wafikie hatua ya kukopa mikopo itakayowanufaisha," alisisitiza Chalamila. Kadhalika, aliiomba Benki ya NMB kuwapunguzia masharti ikiwamo kuwapunguzia riba wakopaji waadilifu wa benki hiyo ambao hukopa na kurejesha mikopo kwa wakati.

Awali akizungumza katika hafla hiyo Kaimu Mkuu wa Idara ya Wateja Wadogo na Kati NMB Makao Makuu, Ally Ngingite, alisema, zoezi la maonyesho ya Siku ya Nyumba na Wajenzi limelenga kuwapa hamasa wananchi kufikia malengo ya kupata mikopo ya ujenzi wa nyumba bora kutoka benki hiyo.

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu, Straton Chilongola, aliwataka wateja wa benki hiyo kutumia fursa ya maonyesho hayo, kujua namna ya kupata mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na kumalizia ujenzi.

# TGNP Mtandao kuendelea na kampeni ya kulinda watoto

**Na Yasmin Protace**

TGNP Mtandao imesema itaendelea na utekelezaji wa kampeni ya ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili wa kingono.

Hayo yalisemwa na Rehema Mwateba, mdau kutoka TGNP Mtandao, alipokuwa akiitambulisha kampeni ya 1_5_5 namlinda, ambapo kampeni hiyo ilifanyika katika Shule ya Sekondari Misitu jijini Dar es Salaam.

Mwateba akizungumza na wanafunzi wa shule hiyo, ambao baadhi yao wapo katika klabu zinazopinga masuala ya ukatili kwa watoto, alisema kuwa kuanzishwa kwa kampeni hiyo, kutasaidiwa watoto kuchukua hatua pale watakapofanyiwa ukatili na pia watakuwa wanaweza kujilinda.

''Kampeni ya 1_5_5 namlinda kuanzishwa kwake kutasaidia kupunguza ukatili, pia kampeni hiyo itawasaidia watoto kuzijua haki zao pale watakapo fanyiwa ukatili," alisema.

Akiongeza kuwa watoto wawe wanatoa taarifa pale wanapofanywa ukatili ili wahusika wachukuliwe hatua.

Aliongeza kuwa matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto yamekuwa yakiongezeka, hivyo kampeni hiyo itasaidia kuwalinda watoto.

Halma Jamil, mmoja wa wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo, alisema kuwa kuanzishwa kwa klabu ya masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia kumewasaidia kujitambua katika kuzijua haki zao.

"Tunaishukuru TGNP Mtandao kwa kuwa mlezi wa klabu yetu na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kunufaika na masuala ya jenda," alisema na kuongeza kuwa klabu yao inawanafunzi 50.

Jackson Massawe, mtaribu wa Jukwaa la Vijana TGNP Mtandao, alisema kuwa TGNP Mtandao, imekuwa mlenzi wa baadhi ya klabu za shule za msingi na sekondari za jijini Dar es Salaam, na kwamba klabu hizo zinazungumzia masuala ya kumlinda mtoto dhidi ya matukio ya ukatili na ukatili wa kingono.

Massawe alifafanua zaidi kwamba kuanzishwa kwa klabu hizo kutawasaidia wanafunzi kuzijua haki zao.

## Wazazi na walezi wahimizwa maadili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI na walezi wa wanafunzi nchini wametakiwa kusimamia nidhamu na maadili kwa watoto wao badala ya kuwaachia walimu pekee jukumu hilo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Jasson Rweikiza, wakati wa mahafali ya 16 ya darasa la saba Shule ya Msingi St Anne Marie Academy yaliyofanyika shuleni hapo, jijini Dar es Salaam.

Alisema ingawa wamekuwa wakiweka bidiii kwenye taaluma na wanafunzi kufaulu kwa viwango vya juu, lakini haitakuwa na maana kama wanafunzi hao watakuwa wakiwa na tabia mbaya.

"Mtafaulu kwenda sekondari hadi vyuo vikuu kwa maksi nzuri sana, lakini kama mtakuwa na tabia mbaya hamtakuwa raia wema ndiyo maana hapa St Anne ibada ni lazima kwa kila mwanafunzi, wazazi tutilie mkazo suala la maadili," alisema Rweikiza.

Alitoa mfano kuwa waliwahi kumfukuza shuleni hapo mwanafunzi wa kidato cha sita baada ya kugundulika kuwa alikuwa akijihusisha na uvutaji wa bangi ili asifundishe wanafunzi wenzake tabia hiyo.

"Huyu mwanafunzi alikuwa akisomeshwa kwa ufadhili wa mtu mmoja ambaye alikuja kumwombea msamaha ili aendelee lakini bodi ya shule ilikataa, hivyo na nyinyi nawaomba msiige tabia za ovyo maana mnaweza kufukuzwa mkaharibu maisha yenu," alisema.

Kuhusu wanafunzi wanaohitimu la saba, Rweikiza aliwahakikishia wazazi na walezi kuwa watafanya vizuri kwenye mtihani yao kwani timu ya walimu wa shule hiyo wamefanyakazi ya kutosha kuwaandaa.

Alisema ushahidi wa hilo ni namna wanafunzi hao ambavyo wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mitihani ya majaribio ya ndani ya shule na wilaya na mkoa wa Dar es Salaam, huku akisisitiza kuwa watafanya maajabu kwenye matokeo kitaifa.

## Ukimwona mzee huyu toa taarifa

**Na Enock Charles**



MZEE wa miaka 80, mkazi wa Kata ya Chikongola Manispaa ya Mtwara Mikindani mkoani Mtwara, Hamis Vulai Hamis, anadaiwa kupotea kwa takribani wiki mbili sasa tangu alipotoweka nyumbani kwake Agosti 6, mwaka huu.

Mtoto wa mzee huyo aliyefika katika ofisi za Nipashe jana, Dadi Hamis, alisema wamemtafuta jijini Dar es Salaam na mikoa mingine ya jirani bila mafanikio baada ya kupata taarifa kuwa mzee huyo alisafiri kuelekea katika jiji hilo.

Alisema wameshatoa taarifa kituo cha Polisi Mtwara na kupewa namba MTR/RB/8401/2019.

Mwenye taarifa kuhusu mzee huyo awasiliane na mtoto wa mzee huyo **0653790004.**

# Msititizo kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa wanafunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WARATIBU Elimu Wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuhakikisha wanawaandikisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari ambao hawana vyeti vya kuzaliwa umri kati ya miaka mitano hadi 18 katika kampeni ya usajili wa vyeti hivyo.

Emmy Hudsoni, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), aliyabainisha hayo jana kwenye mafunzo ya siku moja kwa waratibu elimu kata na maafisa elimu, na kusema kuwa asilimia kubwa ya wazazi wilayani Kahama hawana mwamko juu ya umuhimu wav yeti za kuzaliwa.

Alisema vyeti hivyo vitaweza kuwasaidia wanafunzi wanapomaliza masomo, na kutaka kujiunga na vyuo, majeshi na kupata hati za kusafiria, nakuongeza kuwa wanatarajia kuandikisha wanafunzi 280,000 katika Halmashauri za Msalala,Ushetu na Kahama Mjini.

Alisema kwa kuwa Wilaya ya Kahama inapakana na nchi kadha, hivyo wazazi wanatakiwa kushirikiana na waratibu elimu kuhakikisha kila mwanafunzi anapata cheti cha kuzaliwa ili kupunguza msongamano katika Ofisi ya Mkuu wa wilaya.

Aidha, aliwataka waratibu elimu kuhakikisha wanarejesha fomu za usajili kwa wakati pamoja na kuzifuatilia kwa wazazi mara baada ya kuzigawa ili zoezi la utoaji wa vyeti vya kuzaliwa lisizorote au kukwama.

Mjumbe wa bodi ya Rita, Victoria Lembeli, aliwataka waratibu elimu kuhakikisha wanawasijili wanafunzi na watoto wazaliwa wa Tanzania, na kuongeza kuwa kusajili mtoto ambae sio raia wa Tanzani ni inaweza ikaleta madhara makubwa baadae.

"Raia wa Tanzania huwa anatambulika kuwa na cheti cha kuzaliwa, hii kazi tukiifanya vibaya, matokeo yake mbele ya safari itatuletea madhara makubwa, hivyo inatakiwa tuwe makini wakati wa kampeni hii ya uandikishaji wa wanafunzi wetu," alisema Lembeli.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, alisema atahakikisha anafuatilia zoezi hilo kwa umakini mkubwa, na kutembelea Halmashauri zote za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini kuangalia zoezi linakwendaje.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akikata utepe kuzindua maonesho ya siku mbili ya Siku ya Nyumba, yaliyoandaliwa na Benki ya NMB kwa wateja wake, jijini Mbeya jana. Kushoto ni Maneja Mwandamizi wa Idara ya Wateja Wadogo na Wakati wa Benki hiyo, Ally Ngingite. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vijana CCM wapewa jukumu kumuunga mkono Magufuli

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA mkoani Kilimanjaro wametakiwa kuwa chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi mkoani humo.

Hayo yalisemwa jana mkoani Kilimanjaro na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi ( UVCCM) Wilaya ya Moshi Vijijini, Hassan Salehe Hassan, alipokuwa akizungumza na vijana kwenye uzinduzi wa TPC ya Kijani katika kata hiyo.

Hassan alisema katika kipindi hiki ambacho Rais John Magufuli amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha Tanzania inapiga hatua kiuchumi, ndio wakati pekee wa vijana kusimama na kuhakikisha maendeleo yanafika kila eneo la nchi.

"Nchi yetu kwa sasa ipo kwenye vita ya kiuchumi ambayo inaongozwa na Amri Jeshi Mkuu, Rais wetu Magufuli ambaye amejitolea maisha yake kuhakikisha Tanzania inakua kiuchumi, kazi ya vijana ni kuungana naye ili tuwe na taifa lenye uchumi wa kati," alisema.

"Vijana lazima tufuatilie yote yanayo fanywa na serikali yafanyike kwa umahiri mkubwa na bila kuwa na chembe ya ufisadi, pia tuwe na kazi ya kuwaambia wananchi kile ambacho kinafanywa na serikali ya CCM."

Aidha, katika mkutano huo, Hassan aligawa kanuni za UVCCM kwa lengo la kuwajengea uwezo.

Kwa upande wao baadhi ya madiwani wa Halmashaur ya Wilaya ya Moshi wa CCM, walilalamikia ufisadi unaofanya na viongozi wa kamati ya fedha ambayo inaongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kutumia Sh. milioni 104 za kununulia Ipad badala ya kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

Morris Makoi Diwani wa Ukaoni, akizungumza kwenye mkutano huyo alisema haiwezekani wakanunua Ipd wakati wananchi wana changamoto nyingi katika kata zao.

"Tumekataa kwa hoja ndani ya baraza, lakini wakatumia wingi wao kupitisha hoja hiyo ambayo kiuhalisia ni kama wanajinufaisha wenyewe," alisema.

Aidha, Makoi alimwomba Waziri wa Tamisemi, Seleman Jafo, kuingilia kati suala hilo ili kuokoa fedha za wavuja jasho maskini wanaotozwa kwenye mbege na ndizi zisiende kuwanunulia watu Ipad.

## HABARI ARUSHA

# Vijana wapata elimu afya ya uzazi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

VIJANA katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, wamepatiwa elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango, kwa lengo la kuzuia mimba za ututoni, kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi pamoja na mimba zisizotarajiwa.

Akizungumza katika hafla fupi ya bonanza katika viwanja vya Kata ya Kikatiti, lililowakutanisha vijana kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, Mganga Mfawidhi wa Kliniki ya Chama cha Uzazi bora na Malezi Tanzania (UMATI), Dk. Mariamu Mbaga, alisema waliandaa bonanza hilo, kwa ajili ya kutoa elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango kwa vijana.

Alisema vijana wengi nchini wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango ndio maana walitumia njia ya kuandaa bonanza kwa ajili ya kuwaweka pamoja vijana ili waweze kuwapatia elimu.

Alisema elimu hiyo, inatolewa bure kwenye kliniki zao, kwa mikoa yote miwili na kwa Mkoa wa Arusha wanaitoa siku ya Jumatano ya kila wiki na kwa Mkoa wa Kilimanjaro ni siku ya Ijumaa.

Mwelimisha rika kutoka chama cha UMATI, Jackson Preygod, alisema kabla ya kutoa elimu kwa vijana, kupitia kwenye mabonanza hayo, wanawapatia elimu ya awali.

Hata hivyo, alisema licha ya kutoa elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango, wanawapima elimu ya magonjwa ya kisukari, Ukimwi na saratani bure bila ya gharama yoyote.

Ofisa Mradi wa UMATI, alisema kliniki yao imewalenga vijana kwa sababu ndio nguvu kazi ya taifa kutokana na kuwa wengi ikilinganishwa na makundi mengine.

Alisema mwitikio wa vijana ulikuwa wa kuridhisha na kaulimbiu kuelekea Siku ya Maadhimisho ya Vijana Duniani ni "Kuelekea mwaka 2030, Tanzania ya viwanda, kuboresha elimu kwa maendeleo ya taifa."



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (wa tatu kushoto), akikabidhi zawadi ya Sh. milioni 1.4 kwa mmoja wa askari wa Jeshi la Polisi kati ya saba mkoani humo, mwishoni mwa wiki, fedha ambazo ni sehemu ya Sh. milioni 10 zilizotolewa na serikali, kama pongezi kwa hao, waliokamata madini ya Tanzanite na mengine ya thamani ya Sh. milioni 958 yaliokuwa yakitoroshwa kwenda nchini Kenya mwezi Juni 26, mwaka huu. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Arumeru yapata kifaa kukarabati barabara

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

HATIMAYE kero ya ubovu wa barabara iliyokuwa ikiwakabili wananchi wa Wilaya ya Arumeru, sasa imepatiwa ufumbuzi baada ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Jerry Muro, kupokea mtambo wa kutengenezea barabara aina ya loader. Muro akiongea na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki baada ya mtambo huo kufika, alisema huo ni utekelezaji wa ahadi ya serikali ya utatuzi wa kero sugu ya barabara ambazo zimeharibika na kushindwa kupitika katika wilaya hiyo.

Alisema kutokana na kero hiyo iliyokuwa ikiwakabili wananchi wa wilaya yake kwa muda mrefu, aliamua kutafuta mitambo imara ya ukarabati na matengenezo ya barabara zote za wilaya hiyo, ili wananchi wasiendelee kuteseka na tatizo hilo.

"Mimi kazi yangu nikusikiliza kero za wananchi na kuzitolea ufumbuzi, nilisikiliza kero sugu ya ubovu wa barabara inayowakabili wananchi wa Arumeru na tumeipatia ufumbuzi na ufumbuzi wenyewe ni kama huu wa kuleta kifaa hiki, ambacho tutakitumia pamoja na kile kijiko chetu kwa ajili ya kutengeneza barabara zote za Wilaya ya Arumeru," alisema Muro.

Muro alisema ukarabati rasmi wa barabara hizo utaanza leo kata na vijiji vyote vilivyopo katika Halmashauri ya Meru, pamoja na Arusha DC, zitakarabatiwa.

Alisema kuwa mtambo huo wa barabara aina ya loader umepatikana kutokana na juhudi zinazofanywa na yeye kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, ili kutatua kero zote za wananchi. Akiongea na waandishi wa habari mmoja wa wananchi aliyeshuhudia upokezi wa vifaa hivyo, Loserian Akwi, alisema amefurahi kuona vifaa hivyo, kwa kuwa anaamini tatizo la barabara lililokuwa likiwasumbua kwa muda mrefu limeisha.

"Kwa kweli tumefurahi na tunashukuru sana barabara zetu zilikuwa mbovu mno, yaani hasa katika kipindi cha mvua, lakini naamini hizi mashine zitatuondolea tatizo hili na tutaweza kupitisha bidhaa zetu, bila usumbufu, tunashukuru sana mkuu wetu wa wilaya kwa kutatua kero zetu pamoja na serikali yetu," alisema Agness Kitomari.

# Gambo aagiza polisi kushughulikia vibaka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameagiza Jeshi la Polisi mkoani hapa kuongeza nguvu ya ulinzi maeneo yanayokithiri kwa vibaka pamoja na kukamata vijana wanaotajwa na wananchi wanaojihusisha na kazi hiyo.

Agizo hilo alilitoa mwishoni mwa wiki katika Bwalo la Polisi mkoani hapa, wakati alipokuwa akizungumzia masuala mbalimbali na polisi pamoja na kutoa tuzo ya Sh. milioni 10 iliyotolewa na serikali kwa askari saba waliokataa kuhongwa na watoroshaji madini Juni, mwaka huu, kwenye mpaka wa Namanga wilayani Longido.

Alisema kwa sasa maeneo mbalimbali yamekuwa na vitendo vya kushamiri vibaka, ambao wanakosesha amani wananchi kwa kuwavamia na kuwakata mapanga, kisha kuwapora vitu mbalimbali, huku baadhi yao wakivamia kwenye baadhi ya nyumba na kuiba.

"Sasa hatuwezi kuacha vibaka waendelee kutamba, fanyeni operesheni hasa maeneo yanayojulikana kuongoza kwa vibaka kamateni vijana wote wanaotajwa na wananchi wa maeneo hayo maana wanajulikana waweken ndani na kuwahoji," alisema.

Vile vile, alisema vibaka wanarudisha nyuma jitihada za wananchi, ambao wamejinyima na kutafuta vitu vyao, lakini wajanja wanaotaka kupata kirahisi wanawapora.

Aliagiza askari hao kukamata waendeshaji wa daladala wanaokatisha safari zao zinazojulikana kisheria kama walivyoiandikisha.

"Hawa nao kero kwa wananchi kuna wakati asubuhi au jioni na hasa jioni wanakatisha safari zao na matokeo yake kumpa gharama mwananchi mnyonge kwa kumlazimisha kulipa zaidi, mfano alitakiwa kufika nyumbani kwa kulipa Sh. 400, lakini analazimika kulipa Sh. 1,200 jambo ambalo hatukubali," alisema.

Alisema kitendo hicho ni tamaa mbaya ya wafanyabiashara na kutesa wananchi wanyonge, hivyo lazima ikomeshwe na pia ikiwezekana watakaokamatwa wachukuliwe hatua kali ili kuikomesha. Askari waliopatiwa tuzo hiyo ni Mkuu wa Kituo cha Polisi Namanga, ASP Ernesta Mwambiga, Mkaguzi Msaidizi, Charles Mbawala, Mkaguzi Msaidizi Lameck Mashengele, Koplo Danford, Koplo Peter , PC Erick na PC. Tumaini ambapo kila mmoja amepokea zaidi ya Sh.milioni 1.4 fedha taslimu.

Fedha hizo zimetolewa baada ya kufanikisha kudhibiti madini hayo yasivuke mpaka wa Namanga kwenda nchini Kenya na Waziri wa Madini Dotto Biteko, aliagiza wazawadiwe fedha hizo, ili kuwapa moyo katika uzalendo walioonyesha wa kukataa kuhongwa na watoroshaji madini hayo.

# Mbatia ataka sera moja ya elimu SADC

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWENYEKITI wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, amewapa neno wakuu wa nchi 16 zinazounda Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kuja na ajenda ya pamoja ya sera moja ya elimu inayofanana.

Mbatia amesema kama itakuwapo dhamira ya pamoja ya kuwa na sera hiyo ya elimu kwa wanachama wa SADC, kunaweza kubadili sura ya Afrika na mageuzi makubwa yakaonekana kwa miaka 20 yakisadifu mfumo wa elimu wa nchi za Ulaya. Alizungumza hayo jana, baada ya kumalizika kwa ibada ya misa takatifu ya Jubilee ya fedha ya miaka 25 ya Padri Thomas Salekio Kessy, iliyofanyika katika Kanisa la Mtakatifu Yohani Mtume, Parokia ya Iwa-Kirua Vunjo, mkoani Kilimanjaro. Ibada hiyo iliongozwa na Askofu wa Jimbo Katoliki la Same, Mhashamu Rogathe Kimario, akisaidiwa na Msimamizi wa Jimbo Katoliki la Moshi na Wakili wa Askofu, Deogratius Matiika.

"Kwa mfano, majuzi nilisikia na kusoma baadhi ya maandiko kwamba watu wa Namibia wao wanasema mfano mwanafunzi anayetoka Tanzania na amemaliza kidato cha sita na akienda kwao, kupata Chuo Kikuu kule ni shida, kwa sababu Namibia wao mfumo wao ni mgumu, wao elimu zao wanamalizia kidato cha nne. Unajiuliza hivi silabasi zetu zimeundwa namna gani, nawashauri wakuu wa nchi wanachama ni vizuri tukawa na sera moja ya SADC katika masuala ya elimu," alisema.

Mwaka huu, Tanzania imekuwa mwenyeji wa mkutano wa 39 wa SADC ikiwa imepita miaka 16, tangu mkutano kama huo kufanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2003 chini ya utawala wa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa.

Kuhusu SADC, kuweka mikakati ya kuziwezesha nchi wanachama kufikia malengo ya kuelekea kwenye ukuaji wa uchumi wa kati utakaokuwa na maendeleo ya viwanda, Mbatia alisema:

"Mimi nina ushauri kwa SADC, pamoja na mambo ya viwanda na mambo mengine yote ambayo ni muhimu, wakuu wa nchi 16 wajitahidi sana kuhakikisha nguvu kazi ya SADC ambayo ni vijana, wanapata elimu ambayo ni ujuzi na wanaweza kuzalisha kwenye viwanda, wanaweza kuondoa masuala ya umaskini, njaa, watu wakawa na afya njema lakini penda tusipende ni lazima tuangalie je, mifumo yetu ya elimu ikoje," alieleza. Alisema malengo hayo yanatekelezeka, lakini sharti nchi wanachama wawe wamejiandaa vizuri na kwa utafiti alioufanya, bado kuna kazi kubwa mbele ya safari, na akashauri zaidi kuwa malengo hayo yasiwe ya maneno, yaende kwenye vitendo zaidi.



Balozi wa Kenya nchini Tanzania, Dan Kazungu, akipeana mkono na Mama Maria Nyerere kama ishara ya kutoa salamu katika matembezi ya kihistoria yaliyofanywa na kikundi cha Kenya Maendeleo ya Wanawake Organization (MYWO), ambacho kilianzishwa mwaka 1952 kwa ajili ya kuhamasisha umoja na maendeleo ya wanawake, nyumbani kwa Mama Maria Nyerere, jijini Dar es Salaam. Aliyeketi kulia ni mwanasiasa mkongwe kutoka Kenya, Muthoni Likimani, kushoto ni Rais wa kwanza wa Pan-African Parliament (2004-2009), Getrude Mongella. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matumizi ya Ipad yagawa madiwani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MPANGO wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kununua kompyuta ndogo za mkononi maarufu kama 'Ipad' kwa ajili ya madiwani wake ili kupunguza matumizi ya karatasi na makabrasha yanayotumika kuandaa vikao na taarifa za miradi mbalimbali, umeanza kuwapasua madiwani wake.

Katika mkutano wao na waandishi wa habari juzi, madiwani wanaotoka na Chama Cha Mapinduzi (CCM), Diwani wa Okaoni, Morice Makoi alilalamikia matumizi ya fedha kiasi cha Sh.milioni 104 kuelekeza katika ununuzi wa Ipad, badala ya ukarabati wa barabara za majimbo ya Moshi Vijijini na Vunjo.

"Tunao mfano hapa, kuna fedha zilielekezwa Sh. milioni 104 kwa ajili ya ukarabati wa barabara ambazo zimeharibika kwenye majimbo ya Vunjo na Moshi Vijijini, baada ya mvua za masika kupita. Kilichotokea fedha hizo zimeamuliwa ziende zikanunue Ipad za madiwani pamoja na baadhi ya wataalamu.

"Sasa tumekuja hapa rasmi kutaka kupeleka kilio chetu kuanzia kwa Mheshimiwa Rais John Magufuli, Mkuu wa Mkoa wetu (Dk. Anna Mghwira) na Mkuu wa Wilaya ya Moshi (Kippi Warioba) na viongozi wengine wote ambao wanapenda maendeleo ya nchi yetu.

Bado miezi 10 madiwani waondoke madarakani, katika halmashauri yetu kuna baadhi ya vyoo vimeanguka, zahanati nyingine hazina umeme, leo kuna watu wanachukua milioni 104 wanaamua kwenda kununua Ipad na kununua viti kwa ajili ya ukumbi, wakati viti vipo miaka yote tunakaa."

Makoi ametoa rai kwa serikali iliangalie suala hilo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, atazame kipaumbele cha sasa kama ni wananchi kupata maendeleo ama ni viongozi kujinufaisha kwa vitu ambavyo havina msingi.

Diwani wa Kahe Mashariki, Kamil Mmbando, ameulalamikia mpango huo wa ununuzi wa Ipad hizo, akimwomba Waziri Jafo na serikali yenye dhamana kuzuia jambo hilo.

Alisema unapotaka kumnunulia mtu Ipad kwa miezi hii, maana yake umemnunulia aende akatumie yeye na familia yake na kwamba wao kama madiwani wa CCM, hawawezi kuvumilia ufisadi huo na wanatoa rai na angalizo kwa serikali kuingilia kati suala hilo.

Aidha, Diwani wa Kibosho Magharibi, Deo Mushi, alieleza masikitiko yake kwamba kukiukwa kwa katiba na kanuni za uendeshaji wa vikao vya halmashauri hiyo kunaigharimu serikali.

"Kuja kufanya uchaguzi leo (Ijumaa) siku ambayo haipo katika utaratibu wa vikao vya uendeshaji wa halmashauri, kumeigharimu halmashauri zaidi ya shilingi milioni 3.360, kwa sababu kila mmoja atalipwa. Hizo pesa zingetosha kutumika kwenye barabara, mimi naona huu ni utaratibu mbaya unaoigharimu halmashauri.

Diwani wa Uru Shimbwe, Bertin Mkami, alilalamikia mpango wa upimaji wa viwanja katika eneo la Soko Estate ambalo linatarajiwa kupimwa hivi karibuni, akidai kuwa mpango huo una walakini.

## Familia yahofia vitisho vya usiku

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

FAMILIA moja katika Kijiji cha Tindigani, Kata ya Makiwaru, Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, imetishia kuhama makazi yao kutokana na nyumba wanayoishi kushambuliwa kwa mawe na mchanga nyakati za usiku, huku wanaorusha mawe hayo wakiwa hawaonekani.

Mmiliki wa nyumba hiyo, Wilfred Nassari, anadai kwamba tukio hilo ambalo analihusisha na masuala ya kishirikina, lilianza wiki mbili zilizopita kwa mama yake mzazi anayeishi jirani naye na hatimaye kuhamia kwake.

Habari zaidi kutoka kwa mwanafamilia hiyo, zinaeleza kuwa tangu siku hiyo wamekuwa wakikesha usiku kucha wakisikiliza mashambulizi hayo, lakini wakitoka nje au kuchungulia kujua wanaofanya hivyo ni kina nani, wamekuwa wamwoni yeyote.

"Hayo mawe siku nyingine yanaanza kurushwa kati ya saa 11:00 majira ya jioni hadi saa 6:00 za usiku, na wanaorusha hatuwaoni, jamani hatupati usingizi kutokana na kelele juu ya bati. Tunaomba msaada wa viongozi wa dini wanaoweza kutuombea na kufanya dua ili kuondoa kadhia hii katika familia yetu," ameeleza Nassari.

Kutokana na tukio hilo, Nassari ameeleza namna ambavyo anashindwa kwa sasa kushiriki shughuli za kimaendeleo, hivyo kumlazimu kushinda nyumbani akihofia lolote linaweza kutokea na kuiathiri zaidi familia yake.

"Japo serikali haiamini masuala ya ushirikina, lakini namwomba Mkuu wa Wilaya ya Siha (Onesmo Buswelu) ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na wajumbe wake wafike tu niwaeleze tunachokutana nacho mimi na familia yangu, tumechoka, tunaomba msaada," alisema Nassari.

Kwa upande wake, Elishisa Nassari (68), mama mzazi wa Wilfred alipoulizwa kuhusu kisa hicho alisema: "Tangu kuzaliwa kwangu sijawahi kuona tukio kama hilo, lakini baada ya kujenga nyumba hii mpya ninayoishi sasa, ndiyo tatizo likaanza. Ndugu zanguni tunateseka na watoto wangu na wajukuu zangu, hatulali mawe yanarushwa ovyo kwangu na kwa mtoto wangu wa kiume."

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Tindigani, Musa Jingo, alisema hata yeye amepokea taarifa hizo na kwamba hana uthibitisho kwa kuwa wanaoshuhudia tukio hilo ni familia yenyewe.

Nipashe
Spotika



KUKOSA MAPUMZIKO KUNAVYOTESA NYOTA EPL UK.14



## ISIKUPITE

USHINDI wa Liverpool dhidi ya Southampton juzi, Jumamosi si tu kwamba ulikiweka kikosi hicho cha Jurgen Klopp (pichani) kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, bali pia uliiwezesha kufikia rekodi yao ya kushinda mara 11 mfululizo kwenye mechi za Ligi Kuu, rekodi ambayo mara ya mwisho waliiweka kati ya Februari na April 2014 wakati ikinolewa na kocha Brendan Rodgers.

# HUPATI KITU HAPA!

Kipa na nahodha wa Tottenham, Hugo Lloris, akiruka kupangua krosi dhidi ya beki wa Manchester City, Nicolas Otamendi aliyekuwa akiwania kuukwamisha mpira kimyani kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Etihad na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2 juzi. **PICHA: MTANDAO**

## SOKA




# KUKOSA MAPUMZIKO KUNAVYOTESA NYOTA EPL

**LONDON,** England

NCHINI Uingereza Agosti ni wakati wa mapumziko na familia hutumia muda huo kujumuika pamoja baada ya shule kufungwa.

**Lakini kwa wachezaji wa Ligi Kuu ya England mambo ni tofauti, wachezaji wamerejea kazini, huku kukiwa na hofu huenda wasipate kupumzika kwa karibu miezi 12.**

Mchezaji wa Liverpool, Sadio Mane amegusia suala hilo akisema hajapumzika vya kutosha kwa miaka saba, baada ya kutumia Julai yote kuisaidia Senegal katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika.

Wachezaji wengi wa Ligi Kuu ya England walikuwa mapumzikoni baada ya mechi ya mwisho ya ligi hiyo Jumapili ya Mei 12.

Hata hivyo, baadhi yao walichelewa kwenda likizo hasa wachezaji wa Manchester City na Watford ambao walishiriki fainali ya Kombe la FA wikendi iliyofuata.

Vikosi vya Liverpool na Tottenham pia vilishiriki fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa mjini Madrid Juni Mosi, mwaka huu.

Na hiyo ilikuwa kabla ya michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, Copa America na Kombe Mataifa ya Afrika (Afcon). Mane, alicheza jumla ya mechi 57 nyumbani, Ulaya na zingine za kimataifa katika kipindi cha zaidi ya miezi 11 katika msimu wa mwaka 2018-19.

Hii inamaanisha nyota huyo wa kimataifa wa Senegal wa miaka 27, alianza mazoezi ya msimu mpya Jumatatu ya Agosti 5- siku 17 baada ya kufanya mazoezi yaliyopita

"Nadhani niko tayari," alisema Mane aliyejikuta katika hali kama hiyo miezi 12 iliyopita baada ya kucheza Kombe la Dunia nchini Urusi.

"Sina muda wa kupumzika. Nimekuwa nikicheza kwa muda mrefu. Sijawahi kwenda likizo kwa zaidi ya siku 20 katika kipindi cha miaka saba, lakini nimezoea. Sasa niko tayari. Nipo hapa sasa twende kazi."

Wachezaji wenzake Mane kama vile Alisson, Mohamed Salah, Roberto Firmino na Naby Keita ni baadhi ya wachezaji wa Ligi Kuu walioshiriki mashindano ya msimu wa joto hatua iliyowafanya kukatiza likizo zao kabla ya ligi mpya msimu mpya kuanza.

Lakini kwa wachezaji ambao hawakushiriki mashindano walitarajiwa kufanya mazoezi baada ya msimu kwisha ili kujiimarisha huku wengine wao wakilazimika kwenda likizo na wakufunzi wao kibinafsi.

Kwa mujibu wa mkataba wa Ligi ya England, wachezaji wanastahili kwenda likizo ya "wiki tano ya kulipwa wakati ambao utaamuliwa na klabu-ikiwa mchezaji yuko katika kikosi cha kwanza au anahitajika kushiriki mechi ya kimataifa".

Mazingira ya kazi yao hayawaruhusu kusogeza mbele likizo "Klabu hata hivyo haitamzua mchezaji kuchukua angalau likizo ya wiki tatu bila msingi."

Hilo lingefanikiwa ingelikuwa jambo la kuvutia sana kwa Mane, na mshambuliaji wa Tottenham Son Heung-min ambaye alicheza mechi 78 na kusafiri zaidi ya kilometa 110,000 kuiwakilisha Korea Kusini mwaka uliopita. Muungano wa kimataifa ya takwimu za wachezaji zilionyesha kuwa wachezaji mashuhuri 16 walicheza karibu mechi 80 katika msimu wa mwaka 2018-19.


Likizo ya msimu wa joto huchukuliwa kama likizo ya Sikukuu ya Krismasi na wachezaji barani Ulaya, na baadhi yao hujivinjari mbali na familia na marafiki zao katika migahawa mikubwa kabla ya michezo au siku ya kufungua zawadi.

Jedwali lisilokuwa na muda wa mapumziko limekosolewa sana na Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp na mwenzake wa Manchester City, Pep Guardiola. Klopp alisema: "Ikiwa hatutajifunza jinsi ya kuwasiliana na wachezaji kwa njia bora, wakati wa mashindano, basi huenda tukaangamiza huu mchezo mzuri. Kwa sababu bila wachezaji, hakuna litakalofanyika."

Guardiola anasema michezo ya wakati wa sherehe "inawamaliza" wachezaji wake japo msimu huu angalau watapumzika wikendi moja mwezi Februari, hatua ambayo Shirikisho la Soka limesema ni "muhimu".

Lakini kabla ya kuangazia zaidi maslahi ya wachezaji, ni vema kutilia maanani kuna baadhi ya kazi ambazo watu wanachukua muda mrefu zaidi ofisini ikilinganishwa na mazoezi ya soka.

**JE, WAJUA?**



Pierre-Emerick Aubameyang amefunga mabao saba dhidi ya Burnley kwenye mechi nne alizoicheza Arsenal, ikiwa ni mabao manne zaidi kuliko aliyoifungia timu hiyo katika Ligi Kuu dhidi ya timu nyinginezo.

MICHEZO




# SIMBA ILIVYOBEBA NGAO YA JAMII MARA YA TANO

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya Msudan Sharaf Eldin Shiboub, Mzambia Clatous Chama na Mkenya, Francis Kahata, yaliifanya Simba kutwaa Ngao ya Jamii juzi Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa dhidi ya Azam FC na kuweka rekodi ya kulitwaa mara tatu mfululizo.

**Simba iliachia kipigo cha mabao 4-2, mabao ya Azam yakifungwa na Shaaban Chilunda na Frank Domayo. Huu ni mchezo wa nne sasa Simba kuifunga Azam kwenye mechi ambazo hazihusiani na Ligi Kuu.**

Wakati Simba iliitambia Azam kwenye Ligi Kuu kwa kuifunga mara nyingi, Azam imekuwa mbabe kwa Simba kwenye mechi ambazo zipo nje ya Ligi Kuu. Katika mechi 11 ambazo zimekutana nje ya Ligi Kuu, Azam imeshinda mechi saba, huku Simba ikishinda nne.

Mechi tano ilizoshinda Azam ni za Kombe la Mapinduzi, na mbili ni za Kombe la Kagame.

Aidha, mechi nne ambazo Simba imeifunga Azam, mbili ni za Ngao ya Jamii, kwani mbali na Jumamosi kushinda mabao 4-2, mwaka 2012, Simba iliichapa Azam mabao 3-2 na kutwaa Ngao ya Jamii.

Michuano mingine ni Kombe la Ujirani Mwema. Simba ikishinda mabao 4-3 kwa mikwaju ya penalti baada ya sare ya bao 2-2 mwaka 2012 na pia Kombe la ABC Super 8 mwaka huo huo 2012, ikishinda mabao 2-1.

**HAT-TRICK YA NGAO YA JAMII**

Hii ni mara ya tatu mfululizo kwa Simba kutwaa Ngao ya Jamii, baada ya kuanza kutwaa 2017, 2018 na 2019.

Mwaka 2017 iliifunga Yanga kwa mikwaju ya penalti 5-4 baada ya kwenda dakika 90 bila kufungana, na mwaka uliofuata iliifumua Mtibwa Sugar mabao 2-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, yaliyofungwa na Meddie Kagere na Hassan Dilunga, huku lile la kufutia machozi la Mtibwa likifungwa na Kelvin Sabato.

**YAIFIKIA REKODI YA YANGA**

Ushindi huo wa Simba na kutwaa Ngao ya Jamii mara tatu mfululizo, umeifikia rekodi ya Yanga ambayo ilikuwa ndiyo timu pekee iliyowahi kufanya hivyo nchini.

Awali Yanga ilifanya hivyo mwaka 2013, 2014 na 2015, huku mara zote hizo ikiifunga Azam.

Mwaka 2013, Yanga iliichapa Azam bao 1-0, mwaka 2014, ikaitandika mabao 3-0 na 2015, iliifunga kwa mikwaju 8-7 ya penalti baada ya kutoka sare ya bila kufungana dakika zote 90.

**YAWEKA REKODI YAKE MPYA**

Kwa sasa Simba ndiyo timu inayoshikilia rekodi ya kutwaa Ngao ya Jamii mara nyingi zaidi kuliko timu yoyote ile, kwani imefanya hivyo mara tano.

Mbali na kutwaa mwaka 2017, 2018 na 2019, Simba ilitwaa Ngao ya Jamii mara mbili mfululizo mwaka 2011 na 2012. Iliifunga Yanga 2011 na ikaitwanga Azam mabao 3-2 mwaka 2012.

Timu inayoshikilia nafasi ya pili kwa kutwaa Ngao ya Jamii mara nyingi ni Yanga, iliyofanya hivyo 2013, 2014, 2015. Ilifanya hivyo pia 2001, ilipoifunga Simba kwa mikwaju 3-2 ya penalti baada ya dakika 90 kushindwa kupata mshindi.

**AZAM YAKOSA NGAO YA JAMII MARA TANO**

Timu ya Azam imeweka rekodi ya pekee kwa kuikosa Ngao ya Jamii mara tano, ikiwa ndiyo timu pekee iliyolikosa mara nyingi zaidi baada ya kucheza mechi za kinyang'anyiro hicho, huku ikitwaa mara moja tu.

Azam ilifanikiwa kutwaa Ngao ya Jamii 2016 ilipoifunga Yanga kwa mikwaju 4-1 ya penalti baada ya dakika 90 timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2.

Ilicheza mfululizo mwaka, 2012, 2013, 2014, 2015 mechi za Ngao ya Jamii, lakini ikajikuta inaangukia pua, kabla ya Jumamosi nayo kuchapwa mabao 4-2 dhidi ya Simba.

Mwaka 2012, ilifungwa mabao 3-2 dhidi ya Simba, 2013 ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Yanga, 2014 ikatandikwa mabao 3-0 dhidi ya Yanga, 2015 ikafungwa kwa penalti 8-7 pia na Yanga, kabla ya kutwaa mwaka 2016.

## NJE YA UWANJA

### Benchi laendelea kumhusu Neymar


NEYMAR ameachwa nje kwa wiki ya pili katika kikosi cha Paris St-Germain wakati huu tetesi za mustabali wake wa baadaye hapo Paris zikiendelea kumhusisha na kuondoka.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye alikosa mechi ya ufunguzi ya ligi PSG, dhidi ya Nimes wiki moja iliyopita kabla ya jana tena kutujumuisha katika kikosi kilichoivaa Rennes, amekuwa akihusishwa na kujiunga na Barcelona na Real Madrid.

Hata hivyo, klabu hiyo ya Ufaransa bado haijakubali ofa yoyote kwa Mbrazil huyo.

Kocha Thomas Tuchel alisema "hatakuwa na sisi" Jumapili (jana) katika mechi dhidi ya Rennes, akiongeza kuwa bado hajawa fiti vizuri.

Na wakati Neymar akiweka wazi kuwa mustakabali wake haujaamuliwa, Tuchel alisema: "Kama ninafikiri kuhusu timu imara PSG, ninafikiri timu yenye Ney ndani yake."



## Extra Time



COULIBALY

# MASHABIKI WATAWAKOSA SANA NYOTA HAWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

JUMAMOSI ijayo ndiyo siku ambayo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 utaanza rasmi.

Kwa mujibu wa ratiba ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Namungo FC itaweka historia ya kucheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu, itakapowakaribisha jirani zao Ndanda FC kwenye Uwanja wa Majaliwa mjini Lindi.

**Timu nyingine mpya, Polisi Tanzania nayo itakuwa ikicheza nyumbani kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi dhidi ya Coastal Union, kwenye Uwanja wa Karume mjini Mara, Biashara United itacheza na Kagera Sugar.**

Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, kutakuwa na 'dabi' kati ya timu za mji mmoja, Mbeya City itakapokwaana na ndugu zao Tanzania Prisons, na Uwanja wa CCM Kirumba, Mbao FC itamenyana na majirani zao Alliance FC.

Mechi nzingine zitachezwa Jumapili na zingine baada ya timu za Simba, Yanga, Azam na KMC kumalizia mechi zao za kimataifa.

Pamoja na kwamba kuna wachezaji wapya kabisa ambao wanatarajia kuonekana msimu huu baada ya kusajiliwa na klabu mbalimbali kutoka nje ya nchi, lakini kuna baadhi ya wachezaji ambao wamezoeleka kwa mashabiki wa soka, hawatokuwapo.

Wachezaji hao ni wale ambao walikuwa wakichezea klabu mbalimbali hapa nchini, lakini hawatoonekana tena kwa sababu wamemaliza mikataba na wameondoka, wameachwa au wamesajiliwa na klabu nyingine nje ya nchi.

### 1. KLAUS KINDOKI

Mashabiki wanamkosa sana kipa huyu raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, aliyekuwa akichezea Yanga.

Ni kipa ambaye alikuwa haaminiki sana kwa mashabiki wa Yanga, lakini alikuwa burudani tosha kwa mashabiki wa timu nyingine kutokana na vituko vyake, pamoja na wakati mwingine kufungwa mabao mepesi.

Alikatwa dakika za mwisho na nafasi yake akasajiliwa straika David Molinga ambaye naye pia ni Mkongomani.

### 2. ASANTE KWASI

Beki huyu wa kushoto raia wa Ghana, hatoonekana nchini kwa msimu ujao wa ligi. Alikuwa akiichezea Simba, lakini kabla ya klabu hiyo ameshawahi kuzichezea klabu za Mbao FC na Lipuli ya Iringa.

Ushindani wa namba kwenye kikosi cha Simba ndio uliomwondoa, kwani ameshindwa mara kadhaa jaribio la kupata namba ya kudumu mbele ya Mohamed Hussein 'Tshabalala'. Usajili wa Gadiel Michael pia ukamweka matatani na kuonyeshwa mlango wa kutokea. Kwa sasa amesajiliwa na Baroka FC ya Afrika ya Kusini.

### 3. ZANA COULIBALY

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu unaoanza Jumamosi utamkosa mchezaji mwenye vituko na mbwembwe za aina yake, aliyekuwa kivutio cha mashabiki wengi uwanjani na waliokuwa wakiangalia luninga kumshuhudia Zana Coulibaly raia wa Ivory Coast, aliyekuwa akiichezea Simba, nafasi ya beki wa kulia.

Aina yake ya uchezaji anapopatia, anapokosea, bado imekuwa burudani tosha kwa mashabiki na hata anaposhangilia ushindi.

Ni mchezaji aliyesajiliwa kipindi cha dirisha dogo katikati ya msimu wa 2018/19, lakini akazoeleka na kuizoea Bongo mapema zaidi kuliko wenzake.

Ameachwa kutokana na kutokidhi vigezo, lakini amejiunga na klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Kati ya hawa wote ndiye mchezaji aliyecheza muda mfupi zaidi kwenye Ligi Kuu. Ni miezi sita tu.

### 4. JUUKO MURSHID

Ni beki wa kati aliyekuwa kwa muda mrefu hana mahusiano mazuri na viongozi wa Simba. Mara nyingi viongozi walikuwa wakidai kuwa ni mtovu wa nidhamu. Juuko ni mmoja wa mabeki anayetumia nguvu zaidi kwenye uchezaji wake. Ni tegemeo zaidi kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Uganda, The Cranes kuliko Simba.

Baada ya muda mrefu wa malumbano kati ya viongozi na mchezaji huyo, hatimaye wameachana rasmi na sasa amejiunga na klabu ya Wydad Casablanca ya Moroccco ambayo imekubali kulipa gharama ya mkataba wake uliokuwa unamalizika Novemba mwaka huu. Juuko hatoonekana kwenye Ligi Kuu na klabu ya Simba kwa mara ya kwanza baada ya miaka mitano.

### 5. ABDALLAH SHAIBU 'NINJA'

Beki huyu wa kati wa Yanga, hatoonekana msimu unaokuja baada ya kuitumikia timu hiyo kwa misimu miwili.

Ninja, mchezaji wa Kitanzania ambaye alibezwa mno akitokea klabu ya Jang'ombe, lakini baadaye akatokea kuwa mchezaji tegemeo kwenye klabu hiyo.

Kwa sasa yuko nchini Marekani akiwa amejiunga na klabu ya LA Galaxy kwa mkopo wa mwaka mmoja akitokea klabu ya daraja la tatu ya Jamhuri ya Czech, MFK Karvina aliyosaini mkataba wa miaka minne kama mchezaji huru.

### 6. ELIUD AMBUKILE

Hakucheza mechi nyingi sana msimu uliopita kutokana na mara kwa mara kuwa yupo safarini kwenye majaribio Afrika Kusini na sehemu nyingine, lakini msimu ulipomalizika alikuwa amepachika mabao tisa. Ni mmoja wa mastraika wachache wa Kibongo waliokuwa wakitisha kwenye ufungaji.

Straika huyo tegemeo wa Mbeya City, ni mmoja kati ya wachezaji watakaokumbukwa kwenye Ligi Kuu kwani hatokuwapo na badala yake amejiunga na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

### 7. JAMES KOTEI

Baada ya miaka mitatu, klabu ya Simba na Ligi Kuu ya Tanzania haitokuwa na kiungo mkabaji raia wa Ghana James Kotei, ambaye hakuongeza mkataba na klabu hiyo baada ya kumalizika. Badala yake amekwenda kujiunga na klabu ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Alijiunga na Simba mwaka 2016 akitokea klabu ya Al Orouba ya Oman.

### 8. RAMADHANI SINGANO

Watoto wa mjini wana msemo kuwa ukimpiga teke chura ni sawa na kumwongezea mwendo. Azam FC ilimtangaza kuwa ni mmoja kati ya wachezaji walioachwa kwa msimu ujao wa Ligi Kuu.

Singano, winga za zamani wa Simba, aliwashangaza wengi alipotangazwa kusajiliwa na klabu kubwa ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na kuwa mmoja wa wachezaji wachache wa Kitanzania kusajiliwa na klabu hiyo.

Hatoonekana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya miaka minane, akizichezea klabu za Simba miaka minne na Azam pia miaka minne. Ni mchezaji pekee wa Kitanzania kwenye orodha hii aliyecheza kwa muda mrefu zaidi Ligi Kuu.

### 9. HERITIER MAKAMBO

Ukiondoa Coulibaly, Heritier Makambo raia wa Jamhuri ya Kodemokrasia ya Congo, anafuatia kwa kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa muda mfupi. Amecheza kwa msimu mmoja tu.

Ni mmoja wa mastraika wa kigeni aliyekuwa tishio, akiichezea klabu ya Yanga na kuifungia jumla ya mabao 17 kwenye mechi za Ligi Kuu.

Wanachama na mashabiki wa Yanga watamkumbuka sana, kwani alikuwa kipenzi chao na sasa amesajiliwa na Horoya Athletic Club ya Guinea.

### 10. HARUNA NIYONZIMA

Ni mchezaji wa kigeni aliyecheza Ligi Kuu ya Tanzania kwa muda mrefu zaidi. Kwa mara ya kwanza baada ya miaka minane, Ligi Kuu haitokuwa na mchezaji Haruna Niyonzima.

Kama ilivyokuwa kwa Singano ambaye alipandishwa na Simba na kucheza Ligi Kuu mwaka 2011/12, Haruna alisajiliwa na Yanga akitokea APR mwaka 2011. Aliichezea kwa miaka sita na hadi anaondoka kwenye Ligi Kuu ya Bongo alikuwa akiichezea Simba.

Amejiunga na klabu ya AS Kigali ya nchini kwao Rwanda na kuhitimisha rekodi yake safi ya kuipa ubingwa timu yoyote anayohamia hapa Bongo.

### 11. NICOLAUS GYAN

Ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa kutoka nchini Ghana aliyejiunga na Simba miaka miwili iliyopita akiwa kama straika, lakini alibadilishwa na kuwa beki wa kulia.

Hii ilimfanya kuwa na uwezo wa kushambulia zaidi kuliko kuzuia. Na hata makocha waliokuja nchini kuifundisha Simba wanadhani kuwa ni beki kamili. Hakuna hata mmoja aliyejishughulisha kumrudisha kwenye namba yake ya asili. Simba haijamwongeza mkataba na kuna taarifa kuwa huenda akajiunga na Nkana FC ya nchini Zambia.

### 12. AMISSI TAMBWE

Straika hatari kuwahi kutokea kwenye miaka ya hivi karibuni, Amissi Tambwe hatoonekana kwenye Ligi Kuu baada ya klabu yake ya Yanga kumuacha.

Kwa miaka sita aliyocheza Ligi Kuu Tanzania amekuwa mfungaji bora mara mbili akiwa na Simba msimu wa 2013/14 kwa mabao 19 na 2015/16 akiwa na Yanga, akipachika mabao 21. Tambwe raia wa Burundi mpaka sasa haijajulikana kama amepata timu ya kuichezea nje ya nchi au la.

### 13. EMMANUEL OKWI

Kama isingekuwa kuondoka na kwenda kucheza soka kwenye nchi zingine na kurejea tena nchini mara mbili, Emmanuel Okwi ndiye angeshika namba moja kuwa mchezaji wa kigeni aliyecheza Ligi Kuu kwa muda mrefu zaidi.

Alijiunga na Simba mwaka 2009 akitokea SC Villa, lakini amekuwa klabu yake imekuwa ikimpiga bei na hatimaye kurejea tena nchini.

Hatokuwapo kwenye Ligi Kuu msimu unaoanza kwani baada ya kumaliza mkataba na Simba, kulikuwa na mvutano baina yake na viongozi na ghafla ikatangazwa kuwa amejiunga na Al Ittihad Alexandria ya nchini Misri.

## Nukuu

"Ni hodari sana jinsi anavyocheza na kutamba na mpira na ufungaji wake ni mzuri zaidi. Ni rahisi kumuona mtu kama Raheem [Sterling] akimaliza na mabao kati ya 35 - 40 msimu huu kutokana na jinsi anavyocheza, fursa zinazotengenezwa na Man City na jinsi anavyofunga," **mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Ian Wright.**



"Kujiamini anakohitaji mchezaji hakutoki kwake bali pia hutoka kwa wachezaji wanaomzunguka na kocha. Uhitaji kujisikia kama wewe ni sehemu muhimu ya kundi na [Zinedine] Zidane alinifanya kuwa wa kipekee, amenisaidia sana. Tayari nilikuwa na heshima kubwa sana kwake, lakini kufanya kazi naye kulinifanya kumpenda zaidi," **Cristiano Ronaldo.**




"Mtazamo wake ni mzuri. Alipoumia kifundo cha mguu nilifikiri 'amevunjika', lakini baadaye alifanya mazoezi - (alisema) 'Nipo vizuri na nataka kufanya mazoezi'. Anatuonyesha malengo yake na njaa yake kubwa ya mafanikio. Nafikiri tunahitaji wachezaji kama hawa," **Kocha wa Arsenal, Unai Emery akimzungumzia kiungo Dani Ceballos.**






# STERLING ANAAANZAJE KUFANANISHWA NA MESSI?

**LONDON,** England

RAHEEM Sterling tayari ameshinda Kombe la Ngao ya Jamii msimu huu na anawania kushinda taji la tatu la Ligi Kuu England.

**Huku akiwa amefunga mabao 17 msimu uliopita, manne katika mechi mbili msimu huu- Sterling yuko tayari kwa msimu mwingine bora mwaka huu.**

Mshambuliaji huyu wa Manchester City alikuwa na kampeni ya kipekee msimu wa 2018-19, akichaguliwa na waandishi kuwa mchezaji bora, mchezaji mwenye umri mdogo wa mwaka pamoja na kushirikishwa katika timu bora ya mwaka baada ya mabao yake kuisaidia timu yake kushinda taji la Ligi Kuu katika msimu wa pili mfululizo ambao pia waliweza kushinda mataji matatu.

Pia amekuwa mchezaji muhimu katika kikosi cha Garry Southgate akitajwa kuwa mchezaji maalum na kocha wake, Pep Guardiola na akiwa na umri wa miaka 24, miaka yake bora iko siku zijazo.

Katika kipindi cha BBC Radio 5, Jumatatu usiku - swali liliulizwa iwapo Sterling anaweza kuwa na msimu kama ule wa Messi - mshindi mara tano wa taji la Ballon d'Or na mfungaji mabao 30 na zaidi kila msimu ambaye kila mtu anaweza kujivunia.

Sterling alifunga mabao 25 katika mashindano yote msimu uliopita - yakiwa ndio mabao mengi aliyowahi kufunga katika msimu mmoja na aliendeleza msururu huo wa mabao kwa kufunga hat-trick katika mechi ambayo City iliibuka ushindi kwa mabao matano wakicheza dhidi ya West Ham, kabla ya Jumamosi iliyopita kufunga moja wakitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Tottenham.

Akiwa na umri wa miaka 24 na siku 245 - Sterling alicheza na kutoa mchango kama ule wa Messi wakati mshambuliaji huyo wa Argentina alipokuwa na umri kama huo.

Tofauti iliyopo kuhusu kiwango cha usaidizi wa kila mchezaji alichochangia katika wakati huo si kubwa kwa Messi ikilinganishwa na Sterling, lakini ni ufungaji wa mabao mengi ya Messi ambao unamfanya kuwa mchezaji wa kipekee.

Huku Sterling akifunga mabao 25 msimu uliopita, mabao machache yaliofungwa na Messi katika msimu yake 11 ni 38. Kwa Sterling kulinganishwa na Messi atalazimika kuongeza kiwango chake cha ufungaji maradufu.

"Raheem anaendelea kuimarika," alisema aliyekuwa mshambuliaji wa zamani wa Arsenal, Ian Wright akizungumza na BBC Radio 5 Live.

"Ni hodari sana jinsi anavyocheza na kutamba na mpira na ufungaji wake ni mziuri zaidi. Ni rahisi kumuona mtu kama Raheem akimaliza na mabao kati ya 35 - 40 msimu huu kutokana na jinsi anavyocheza, fursa zinazotengenezwa na Man City na jinsi anavyofunga."

Wakati Manchester City ilipomsaini Sterling kutoka Liverpool 2015 kwa dau la pauni milioni 49, alikuwa mchezaji ghali zaidi kutoka Uingereza.

Thamani yake ilitokana na shinikizo nyingi kwa mchezaji mwenye umri wa miaka 20 na pengine haishangazi ni kwa nini Sterling hakuweza kuonyesha mchango wake alitaka kutoa.

Lakini mtu mmoja ambaye hakuwa na wasiwasi naye ni kocha, Pep Guradiola.

Msimu wa 2016, wakati Sterling alipokuwa na msimu mbaya wa Ulaya ambapo alitolewa baada ya kipindi cha kwanza akiichezea England dhidi ya Wales kufuatia kipindi kibaya cha kwanza, alipokea ujumbe katika simu yake uliosema: "Usijali najua wewe ni mchezaji mzuri, utakaponifanyia kazi, nitakupigania".

Ujumbe huo ulitoka kwa mkufunzi wake mpya wa klabu ambaye alimtambua Sterling kama mchezaji mwenye kipaji cha kuwa mchezaji bora sawa na Messi.

Katika msimu wake wa pili akishirikiana na Guardiola, Sterling alifunga mabao 23 - ikiwa ni mara mbili ya aliyofunga katika msimu yake sita aliyocheza soka la kulipwa.

Kama Sterling, ufungaji mabao wa Messi kabla ya kucheza chini ya ukufunzi wa Guardiola ulikuwa mzuri, lakini sio bora - alifunga mabao 16 katika kipindi cha msimu wa 2007-08.

Lakini msimu uliofuata aliongeza idadi hiyo na kufikia 38. Kwa Sterling kuweza kujumuishwa na kulinganishwa na Messi idadi yake ya mabao itahitaji kuimarika zaidi.

Uimarikaji huo uliambatana na hatua ya Guardiola kumchezesha Messi kama mshambuliaji wa katikati na pia ameweza kumchezesha Sterling katikati katika mechi ya maandalizi ya msimu huu, ambapo Sterling alifunga mabao matano.

"Amejitahidi vilivyo na imani yake imeongezeka kwa kile ambacho amekuwa akifanya katika mazoezi. Sasa atakuwa akivunjika moyo kwa kufunga mabao matatu na kushindwa kufunga bao moja zaidi kwa sababu hilo ndio lengo lake sasa. Anataka kuongeza idadi ya magoli yake."

**NAJUA WAJUA**



HII ni mara ya kwanza Liverpool kushinda mfululizo mechi zake mbili za kwanza kwenye zama za msimu wa Ligi Kuu England tangu ianze kuitwa Premier League, katika kipindi cha hivi karibuni kuwahi kufanya hivyo ilikuwa msimu wa 1993-94 na 1994-95.

SOKA




# JEZI ZINAVYOZITAJIRISHA KLABU LIGI KUU ENGLAND

**LONDON,** England

WADHAMINI wa Manchester United kwenye jezi zao, Chevrolet bado wanashika namba moja kwa kutoa mkwanja mrefu kwenye Ligi Kuu England kwa mujibu wa mwandishi wa habari, Alex Miller.

**Dili hilo la udhamini waliloingia Man United na kampuni hiyo ya watengeneza magari mwaka 2012, linatajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 64 kwa mwaka.**

Hiyo ina maana kwamba Man United inavuna pauni milioni 64 kila mwaka kutokana na jina la Chevrolet kutokea kwenye jezi zao.

Wadhamini wa kwenye jezi za Brighton, American Express ndio wanaolipa fedha kidogo zaidi kuliko wote kwenye Ligi Kuu England, pauni milioni 1.5 kwa mwaka.

Lakini, wadhamini hao wapo kwenye ubia pia na Seagulls, ambao pia wanamiliki haki ya jina la uwanja wa nyumbani wa timu hiyo.

Lakini, kwenye mgao huo wa fedha za wadhamini kwenye jezi umeonyesha wazi tofauti iliyopo baina ya klabu sita bora na nyingine.

Kwa mfano tu, dili la West Ham United na Betway linashika namba saba kwa ukubwa, lakini ni kama asilimia 28.6 ya mkwanja wanaovuta Tottenham Hotspur kupitia wadhamini wao AIA ambao wapo kwenye namba sita.

Wadhamini 10 kati ya 20 walipo kwenye timu za Ligi Kuu England msimu huu ni makampuni ya kamari. Kiongozi msaidizi wa Chama cha Labour, Tom Watson amedai kwamba atazizuia timu kusaini dili za udhamini na makampuni ya kamari hapo baadaye kama chama chake kitaingia madarakani.

Lakini wadhamini wanaotamba kwenye Ligi Kuu England wengi ni makampuni ya kutoka Asia, huku shughuli zao nyingi zikifanyika nje ya Uingereza.

Hii hapa orodha ya wadhamini wakuu wa kwenye jezi za Ligi Kuu England na mkwanja wao wanaotoa kwa mwaka.

Man United wanavuna pauni milioni 64 kupitia Chevrolet, wakati wapinzani wao Manchester City wanavuna pauni milioni 45 kupitia udhamini wa Etihad, huku Arsenal wakishika namba tatu kwa kuingiza pauni milioni 40 kupitia Emirates, kiwango sawa wanacholipwa Chelsea kupitia Yokohama na Liverpool kupitia Standard Chartered.

Chelsea na Liverpool kila moja zinavuna pauni milioni 40 kwa mwaka kupitia wadhamini wao wakuu kwenye jezi. Sita bora inakamilishwa na Spurs, ambao wanavuna pauni milioni 35 milioni kupitia AIA.


West Ham wao wanavuna pauni milioni 10 kupitia Betway, huku Everton wakishika namba nane wakivuna pauni milioni 9.6 kupitia SportPesa, wakati Wolves wanavuna pauni milioni nane kupitia ManBetX na Southampton wanakamilisha 10 bora wakivuna pauni milioni 7.5 kupitia wadhamini wao LD Sports.

Burnley wanavuna pauni milioni 7.5 kupitia wadhamini wao LoveBet, wakifuatiwa na Crystal Palace wakivuna pauni milioni 6.5 kupitia wadhamini wao ManBetX, sawa na kiwango wanachovuna Newcastle United kupitia Fun88 na Watford wakivuna kupitia Sportsbet.io.

Aston Villa wanavuna pauni milioni sita kupitia W88, wakati Bournemouth wanaweka mfukoni pauni milioni tano kwa udhamini wa M88, huku Leicester City wanaingiza pauni milioni nne kwa udhamini wa King Power, Sheffield United pauni milioni 3.5 kupitia USG, Norwich City pauni milioni tatu kupitia Dafabet na Brighton wakiweka kibindoni pauni milioni 1.5 kupitia wadhamini wao wakuu kwenye jezi American Express.

HARRY MAGUIRE

NDANI YA 18



SADIO Mane ni mchezaji wa kwanza kufunga mara nne mfululizo kwenye mechi za ufunguzi za msimu wa Ligi Kuu England tangu Mark Viduka alipofanya hivyo kati ya msimu wa 2002-03 na 2005-06.




JUMAMOSI ijayo ndiyo siku ambayo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20 utaanza rasmi. Kwa mujibu wa ratiba ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Namungo FC itaweka historia ya kucheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu...

Uk. 16&17



UPAMECANO

# YOSSO WA KUTAZAMWA BUNDESLIGA MSIMU HUU

**MUNICH,** Ujerumani

LIGI Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, imekuwa ligi inayopendwa na wachezaji wachanga wanaotaka kuimarika kimchezo. Huku ikiwa Jadon Sancho na Kai Havertz washajijengea majina, wachezaji wengi chini ya umri wa miaka 21, sasa wako tayari kuibuka.

Makala hii inakuchambulia wachezaji chipukizi wa kuchungwa Ligi Kuu ya Ujerumani.

**KAI HAVERTZ, 20- BAYER LEVERKUSEN**

Nyota wa kizazi kijacho cha Ujerumani. Havertz ashacheza mechi 88 katika Ligi Kuu ya Ujerumani na kufunga mabao 24. Ana ujuzi wa ajabu wa kiufundi, anacheza kwa miguu yote miwili na ana uwezo wa kuunda nafasi za kufunga na kufunga mwenyewe. Havertz amesema atasalia kuwa mchezaji wa Leverkusen msimu huu ingawa ni wazi kuwa hatocheza hapo kwa muda mrefu. Bayern Munich wamevutiwa naye kwa muda mrefu.

**JADON SANCHO, 19- BORUSSIA DORTMUND**

Wengi walitaka kujua itakuaje kijana Muingereza kucheza Ujerumani, sasa ni kielelezo chema huku chipukizi wa Uingereza wakitaka kufuata nyayo zake. Winga huyo wa zamani wa Manchester City ana uwezo mkubwa na anafanya maamuzi mazuri kuzidi umri wake, ana kasi na amemakinika. Baada ya kupewa nafasi msimu wa 2017-18, alikuwa mmoja wa nyota msimu uliopita akifunga mabao 12 na kusaidia mengine 17.

**DAYOT UPAMECANO, 20- RB LEIPZIG**

Beki huyo wa kati wa Ufaransa ni mwingine anayetazamiwa kufika kileleni. Upamecano ni mahiri kwa mipira ya kichwa na anasoma mchezo vema. Anaweza pia kupeleka mipira katika kiungo cha kati. Amekuwa mmoja wa mabeki bora katika Ligi ya Ujerumani. Julian Nagelsmann atakuwa kocha mzuri kwake.

**IBRAHIMA KONATE, 20- RB LEIPZIG**

Beki mwingine wa kati wa RB Leipzig ambaye anaweza kucheza vema kwa mipira ya kichwa na chini. Konate alikuwa na msimu mzuri uliopita na aliishikilia nafasi yake vema baada ya Upamecano kupata jeraha mwishoni mwa msimu. Chipukizi huyo wa Ufaransa amemwelezea Upamecano kama kaka yake na watatarajia kuendeleza mchezo wao wa kuridhisha msimu huu.

**ALPHONSO DAVIES, 18- BAYERN MUNICH**

Winga huyo wa Canada alizaliwa katika kambi ya wakimbizi na akajiunga na Bayern Januari mwaka huu. Alishiriki mechi kadhaa kama mchezaji wa akiba na kwa ujumla alicheza dakika 74 na akafunga bao lake la kwanza dhidi ya Mainz. Kuondoka kwa Arjen Robben na Frank Ribery huenda kukatoa nafasi zaidi kwa Davies msimu huu hasa baada ya mchezaji aliyelengwa kusajiliwa na Bayern, Leroy Sane kuwa majeruhi pale Man City na kukatisha mpango huo.

**MARCUS THURAM, 21- GLADBACH**

Mtoto wa bingwa wa zamani wa dunia na Ufaransa, Lilian, alijiunga na Monchengladbach Julai baada ya kuridhisha katika Klabu za Ufaransa Sochaux na Guingamp. Kinyume na baba yake ambaye alikuwa mmoja wa mabeki mahiri wakati wake, Marcus ni mshambuliaji na anapenda kucheza katika wingi ya kushoto. Ana uwezo mkubwa wa kutamba na mpira na anaweza kupewa jukumu la Thorgan Hazard aliyehamia Dortmund.

**WESTON MCKENNIE, 20- SCHALKE**

Nyota iliyong'ara katika msimu wa kiza wa Schalke. Mckennie alikuwa nahodha wa Marekani katika mashindano ya Gold Cup msimu wa majira ya joto licha ya umri wake mdogo. Alicheza katika nafasi tofauti msimu uliopita wakati kocha wake Domenico Terdesco alipojaribu kutafuta mbinu ya kushinda ambayo hakuipata. McKennie amemkaribisha Mmarekani mwenzake David Wagner ambaye ameteuliwa kuwa kocha.

**EVAN N'DICKA, 19- EINTRACHT FRANKFURT**

Mfaransa mwingine N'Dicka aling'ara hakuzungumziwa sana msimu uliopita kwa kuwa washambuliaji watatu wa Frankfurt ndio waliogonga vichwa vya habari. Lakini beki huyu wa kati alikuwa na mchezo mzuri katika nusu ya pili ya msimu ambapo alishinda tuzo ya mchezaji bora chipukizi kucheza mara ya kwanza katika Bundesliga Februari mwaka huu.

**JOSH SARGENT, 19- WERDER BREMEN**

Mshambuliaji huyu wa Marekani aling'ara mara alipopewa nafasi msimu uliopita ambapo alifunga kwa kichwa dakika mbili baada ya kuingia kama mchezaji wa akiba katika mechi yake ya kwanza. Alimaliza msimu na mabao mawili kwenye ligi baada ya kucheza kwa dakika 205 tu na licha ya kukosa kutajwa kwenye kikosi cha Marekani cha Gold Cup kocha wake wa Bremen Florian Kohfeldt ameridhika naye.

**ADEMOLA LOOKMAN, 21- RB LEIPZIG**

Mmoja wa Waingereza waliofuata nyayo za Sancho, Lookman alikuwa na msimu mzuri alipokuwa kwa mkopo Leipzig. Mshambuliaji huyo anacheza sehemu yoyote ya mashambuliaji na ni mfungaji ambapo alifunga mabao matano katika dakika 574 alizopata. Klabu yake ya Everton ilimkubalia ajiunge na Leipzig kwa kandarasi ya kudumu baada ya kupata nafasi finyu za kucheza hapo Goodison Park.

**RABBI MATONDO 18- SCHALKE**

Winga huyo wa Wales amefuata nyayo za Sancho kutoka Man City na amejiunga na Schalke kwenye Bundesliga. Ilisemekana kwamba ndiye mchezaji mwenye kasi zaidi Man City, Matondo alifanikiwa kuingia mara kadhaa kama mchezaji wa akiba hapo Schalke mwaka jana. winga huyo atatarajia kupata nafasi nyingi zaidi za kucheza msimu huu.

**USILOLIJUA**

Alexandre Lacazette amehusika moja kwa moja katika mabao 28 (mabao 21 na pasi za mwisho saba) kwenye mechi 36 za Ligi Kuu England alizoichezea Arsenal katika Uwanja wa Emirates.



# Serikali yabaini utoroshaji dhahabu

Na Nebart Msokwa,
CHUNYA

WAKATI serikali ikipambana kudhibiti utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi, imebainika zaidi ya nusu ya dhahabu inayonunuliwa na wanunuzi wa kati maarufu kama 'brokers' kutoka kwa wachimbaji wadogo wilayani Chunya inatoroshwa.

Akizungumza na wanunuzi wa dhahabu wilayani Chunya, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhandisi Maryprisca Mahuli, alisema wamefanya uchunguzi na kubaini kuwa kiasi kikubwa cha dhahabu inayonunuliwa kutoka kwa wachimbaji wadogo hakipelekwi kwenye soko kuu lililofunguliwa wilayani humo.

Alisema licha ya soko la madini lililofunguliwa wilayani kufanya vizuri, lakini kiasi kikubwa cha dhahabu inayouzwa sokoni hapo ni ile inayotoka kwenye viwanda vya uchenjuaji wa dhahabu, huku dhahabu inayonunuliwa kwa wachimbaji wadogo ikiwa haijulikani inakouzwa.

"Tumefanya uchunguzi na tumegundua ni kiasi kidogo sana cha dhahabu inayouzwa kwenye soko letu kinatoka kwa wachimbaji wadogo wanaotumia mercury (zebaki) kuisafisha na tumebaini kuwa kiasi kikubwa cha dhahabu hiyo, inayonunuliwa na wanunuzi wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo inatoroshwa," alisema Mahundi.

Alisema katika uchunguzi huo tayari amepata orodha ya wanunuzi wote wanaotorosha madini nje ya wilaya hiyo, hivyo atawaita kila mmoja kwa nafasi yake ili ajieleze kuwa anatorosha madini na kuikosesha serikali mapato.

Alisema kitendo cha kutorosha madini sio tu kinaikosesha serikali mapato, bali pia ni cha uhujumu uchumi, na kuwaonya wanunuzi hao kuacha tabia hiyo mara moja.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Wilaya ya Chunya, Lutufyo Mwambungu, alisema utoroshaji huo wa dhahabu una harufu ya kuambatana na vitendo vya rushwa.

Mwambungu aliwataka wachimbaji, wanunuzi na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa ya vitendo hivyo kwenye vyombo vya dola ili hatua zichukuliwe kukomesha tabia hiyo.

Naye Ofisa Madini Mkazi wa Wilaya ya Chunya, Gibson Kamihanda, aliwataka wale wote wanaojihusisha na utoroshaji wa dhahabu kuacha tabia hiyo mara moja kwa vile adhabu yake kisheria ni kali kiasi cha kuwafilisi na kuwaondoa kabisa kwenye biashara ya madini.

Alisema kwa mujibu wa sheria mtu akikutwa anatorosha madini, hatua ya kwanza madini hayo yataifishwa, atatakiwa kulipa faini ambayo ni mara tatu ya thamani ya madini aliyokutwa nayo pamoja na tozo zote ambazo madini hayo yangelipiwa kama yangeuzwa kwa njia halali.

Alisema kuwa kwa sasa hakuna haja ya kutorosha madini hayo kwa vile bei elekezi ya soko inaakisi bei ya dhahabu kwenye soko la dunia na kwamba hata kama mtu akienda kuuza mahali pengine hawezi kupata bei nzuri zaidi ya ile inayopatikana kwenye soko kuu la madini lililofunguliwa na serikali wilayani humo.

Kwa upande wake Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wilaya ya Chunya, Osaund Mbilinyi, alidai kuwa ipo changamoto ya wanunuzi na wachimbaji wa madini kutokuwa na mwitikio wa kulipa kodi.

Alisema maofisa wa TRA wapo kwenye soko la dhahabu la Wilaya ya Chunya na wanunuzi na wachimbaji wa dhahabu anapofika hapo hupewa elimu na kasha kukabidhiwa fomu ambazo wanapaswa kuzijaza ili maofisa hao waende kwenye maeneo yao ya kazi kuwakadiria kodi, lakini wengi wao wamekuwa hawarejeshi fomu hizo na kuingia mitini.



Mbunge wa Bukoba Vijijini (CCM), Dk. Jasson Rweikiza (wa pili kulia), akikabidhi cheti kwa mmoja wa wanafunzi wa Shule ya St Anne Marie Academy ya Mbezi Kwa Msuguli, katika mahafali ya darasa la saba yaliyofanyika shuleni hapo, jijini Dar es Salaam wikiendi. Kulia ni Mkuu wa Shule hiyo, Gladius Ndyetabura na (wa tatu kulia) ni Kaimu Mratibu wa Shule, Venance Rwegoshola. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Walimu masomo ya sanaa watoa angalizo

Na Nebart Msokwa,
UNGWE

WAKATI serikali ikihamasisha wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi na Hisabati, walimu wa masomo ya Sanaa wilayani Rungwe wamelalamikia utaratibu huo wakidai masomo ya Sanaa kwa sasa yanakosa wanafunzi.

Inadaiwa baadhi ya wanafunzi wanaofaulu kidato cha nne na kutakiwa kujiunga kidato cha tano kwenda kusoma masomo ya michepuo ya Sanaa, wanabadili michepuo hiyo na kujiunga na masomo ya Sayansi.

Wakizungumza kwenye hafla ya kuwapongeza walimu na wanafunzi waliofanya vizuri kwenye mitihani ya kidato cha sita mwaka huu, walimu hao walisema hali hiyo inafanya walimu wa michepuo ya wanafunzi wa michepuo ya Sanaa kukosa wanafunzi.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Rungwe, George Makweta, alisema kuna wimbi kubwa la wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na masomo ya Sanaa kutaka kubadili masomo hayo wakidai masomo hayo hayana faida kwao. Alisema hali hiyo inaweza ikawa na madhara makubwa kwa taifa baadaye, hivyo akaishauri serikali kuondoa utaratibu wa kuwaruhusu wanafunzi kubadili michepuo wanayochaguliwa nayo.

"Kwa sasa kumeibuka tatizo kubwa la wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga kidato cha tano na masomo ya Sanaa kutaka kubadili na kusoma masomo ya Sayansi, wanasema kabisa kwamba masomo ya Sanaa hayana faida yoyote kwao," alisema Makweta. Aliomba serikali kuangalia namna bora ya kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo hayo kwa madai kuwa endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kuna hatari ya kutokea tatizo baadaye.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, aliwashauri wazazi kuwaelimisha watoto wao mapema ili wajue wanapoenda shuleni wanaenda kusoma masomo gani na kwa malengo gani ya maisha yao.

Alisema hiyo itasaidia kuwa na usawa wa wanafunzi kwenye masomo yote na kuepuka changamoto hiyo ya wanafunzi kuyakimbia masomo ya Sanaa.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya hiyo, Abel Ntupwa, alisema kuna kazi kubwa ya kufanyika katika wilaya hiyo, ili matokeo ya kidato cha nne na cha sita yaendane kwa madai kuwa kwa sasa hayaendani.

Alisema kwa mwaka huu ufaulu wa kidato cha sita umefikia asilimia 90 wakati ufaulu wa kidato cha nne uko kati ya asilimia 80 na 85, hivyo akashauri juhudi iongezwe ili ufaulu huo uendane.

Ofisa Elimu Taaluma wa Mkoa wa Mbeya, Oscar Msabaha, alisema pamoja na kwamba kazi ya walimu ni kufundisha, lakini pia ndio walezi wa watoto.

# Usajili NGO sasa wasuasua

Na Nebart Msokwa, MBEYA

ZOEZI la usajili wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGO) mikoa ya Nyanda za Juu Kusini limefanyika kwa kusuasua kufuatia mwitikio wa mashirika hayo, kujitokeza kusajiliwa kuwa mdogo.

Hali hiyo inatokea licha Ofisi ya Msajili wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuhamasisha.

Zoezi hilo lilifanyika jijini Mbeya ambapo maofisa wa Wakala wa Usajili Leseni na Biashara (Brela), Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) pamoja na maofisa wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi walikuwa wakiendelea na zoezi, huku wadau wa mashirika wakiwa wachache.

Msemaji wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii), Erasto Ching'on, alisema lengo la zoezi hilo ni utekelezaji wa matakwa ya kisheria ambayo yanataka mashirika yote kuhuisha taarifa zake.

Alisema pamoja na umuhimu wake, lakini bado wenye mashirika hayo wanasuasua kujitokeza kuhuisha taarifa hizo, hivyo akawataka kujitokeza mapema kabla zoezi hilo halijafikia ukomo.

"Mabadiliko ya Sheria ya Mashirika ya Kijamii namba 3 ya mwaka 2019 yanataka mashirika ya kijamii ambayo awali yalisajiliwa na Brela na Rita kujisajili Ofisi ya Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili taarifa zao ziweze kutambulika katika mfumo mmoja," alisema Ching'on.

Alisema baada ya zoezi hilo kufikia tamati mashirika ambayo yatakuwa hayajahuisha taarifa zake, yatapewa miezi miwili na baada ya hapo endapo yatakuwa hayajasajiliwa yatakuwa yamejiondoa kwenye utoaji wa huduma.

Alisema kuwa lengo la kufanya usajili kwa mashirika ni kuimarisha utawala bora, uwazi na uwajibikaji na kutambua michango ya mashirika hayo katika sekta mbalimbali za kijamii hususan afya, elimu pamoja na mambo mengine ya maendeleo.

Mwakilishi wa Shirika la Wasaidizi wa Kisheria Wilaya ya Mbeya (MBAPAO), Musa Magullu, alisema changamoto ni namna ya ushirikishwaji katika kufanya maamuzi, na kwamba wamefika hapo hawatambui ni nini cha kufanya.



# Takukuru yaagizwa kufanya uchunguzi daraja Kingale

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa mkoani Dodoma (Takukuru), imeagizwa kufanya uchunguzi wa mradi wa ujenzi wa daraja la Kingale Wilaya ya Kondoa baada ya kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kutilia shaka mradi huo.

Kiongozi huyo Mzee Mkongea Ally, aligoma kuuzindua na kuiagiza taasisi hiyo kufuatilia ndani ya wiki mbili baada ya kukosekana nyaraka za taarifa zote zinazotakiwa kuwapo wakati wa ukaguzi wa mradi huo. Akizungumza baada ya kutembelea mradi huo, Ally alisema Takukuru inatakiwa kufanya uchunguzi ndani ya wiki mbili ili kuwasilisha makao makuu kile walichobaini kwa ajili ya kuhakikiwa ili mradi huo upate nafasi ya kuzinduliwa.

Alisema baada ya uchunguzi wao kukamilika Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, atapanga nafasi nyingine kwa ajili ya kwenda kuzindua kama inavyotakiwa kufanywa.

"Takukuru naomba mfanye kazi yenu na muwasilishe taarifa makao makuu ili ifanyiwe kazi na kutolewa majibu stahiki," alisema Ally. Alisema lengo lao ni kujiridhisha na taarifa iliyotolewa pamoja na kutaka miradi inayotolewa na serikali itekelezwe kwa ufanisi ili kuwa na manufaa kwa wananchi.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wa Halmashauri ya Kondoa Mji, Brithon Kimaro, alisema mradi huo wa barabara na daraja umegharimu Sh. milioni 165.2, huku daraja pekee likigharimu Sh. milioni 138.2 ambazo zimetumika kwa ajili ya matumizi ya ujenzi.

Kimaro alisema fedha hizo ni za serikali ambazo zimetoka kwenye mfuko wa barabara kwa lengo la kuboresha miundombinu hiyo, ili kurahisisha utoaji huduma ya usafiri kwa wakazi wa eneo hilo.

Alisema mradi huo ni muhimu kwa jamii kwa sababu unakwenda kutoa huduma ya mawasiliano baina ya sehemu moja kwenda nyingine jambo ambalo ni muhimu kulitekeleza ili wananchi waendeshe shughuli zao za kiuchumi kiurahisi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kondoa, Sezaria Makota, alisema maagizo yaliyotolewa yatatekelezwa ipasavyo ili kuhakikisha mradi huo unaendelea kutekelezwa na kufanikisha maendeleo ya wakazi wa eneo hilo.

Alisema daraja hilo ni muhimu kwa wananchi kwa sababu linasaidia wakazi wa eneo la Kingale kupata huduma ya usafiri kirahisi pindi litakapokamilika ikiwamo kusaidia kufanya shughuli za biashara kirahisi kupitia barabara hiyo.



Wajane kutoka vijiji vya Wilaya ya Nachingwea, wakimsikiliza Ofisa Tarafa ya Nambambo, Christopher Mkuchika (hayupo pichani), baada ya kupokea misaada mbalimbali iliyotolewa na huduma ya kiroho kwa watu wasiofikiwa kutoka kanisa la EAGT Ipagala, Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# BHM kuanza upandikizaji uboho mwakani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) ipo katika hatua za mwisho kuingia makubaliano na chuo kikuu kimoja nchini Italia kwa ajili ya kushirikiana katika matibabu ya upandikizaji wa uboho.

Hayo yalielezwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonse Chandika, alipokuwa akitoa maelezo kwa wajumbe wa Baraza Kuu Taifa la Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT), walipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015-2020.

Alisema huduma hiyo (bone narrow transplant), itaanza kutolewa hospitalini hapo mwakani.

"Tutaanza upandikizaji wa uboho mwakani. Upandikizaji wa uboho unasaidia katika matibabu ya selimundu," alibainisha.

Dk. Chandika alisema: "Tayari watumishi wetu wameshaanza kupata mafunzo ya upandikizaji wa uboho. Kuna ambao wameenda Italia kwa ajili ya mafunzo na ambao wanapokea mafunzo kupitia telemedicine."

Alisema hospitali hiyo imeshafanya upandikizaji wa figo kwa watu saba ikiwa ni miaka mitatu tangu kuanzishwa kwake.

Alisema lengo la hospitali hiyo ni kutoa huduma kama hospitali ya rufani ya kanda na kuwa hospitali ya pekee ya kutoa huduma za kibingwa ambazo awali zilikuwa hazipatikani nchini.

"Hapa tunatoa huduma ya figo, moyo, macho, saratani na huduma ya upasuaji wa matundu madogo, katika figo, tumeshapandikiza figo kwa wagonjwa saba na wanaendelea vizuri, alisema Dk. Chandika.

Alieleza kuwa wanafanya kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na wataalamu kutoka nchini Japan kwa ajili ya kuwafundisha wataalamu wa ndani ili wazawa waweze kutoa huduma hizo.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa UWT Taifa, Jesca Mbogo, alipongeza mafanikio makubwa ya huduma za afya zilizopatikana ndani ya muda mfupi katika hospitali hiyo na kupunguza mzigo kwa serikali wa kupeleka watu nje ya nchi kwa matibabu.

Mbogo alipongeza serikali kwa uwekezaji mkubwa wa kujenga hospitali ya kisasa hivyo kuimarisha huduma za afya nchini.

Hata hivyo, alitoa rai kwa kinamama kujenga utaratibu wa kupima afya zao mara kwa mara ili kupata tiba mapema na kwa wakati.

Alisema serikali imefanya jitihada kubwa ya kuwekeza katika sekta ya afya kama ilani ilivyoelekeza, hivyo ni wajibu wa kinamama kujitokeza kupima magonjwa mbalimbali yakiwamo yasiyoambukiza ili wapate ushauri na tiba mapema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wajumbe hao waliushukuru uongozi wa UWT kwa kuwawezesha kuona mambo mazuri yanayofanywa na serikali kwa kuwa mwanzoni waliyajua kupitia vyombo vya habari.

"Ziara hii imetuonyesha mambo ambayo serikali imeyafanya kwa wananchi wake, kikubwa ni kuwaomba wananchi waunge mkono serikali yao," alisema Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dodoma, Neema Majule.

Mwenyekiti wa UWT Kusini Unguja, Shamsa Abdallah Ally, alishukuru uwapo wa Muungano uliowawezesha kufika Bara na kujionea mambo yaliyofanyika na kutoa wito kwa wawekezaji kujitokeza zaidi kuwekeza Dodoma.

# Halmashauri 100 kikaangoni miradi ya afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI za wilaya 100 zimetakiwa kujieleza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), kutokana na kusuasua kwenye utekelezaji wa miradi ya afya iliyopo chini ya Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Ukimwi, Kifua Kikuu na Malaria.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akifunga kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa shughuli za mfuko huo, jijini hapa.

Alisema halmashauri 85 zimefanya vizuri kwenye utekelezaji wa mradi huo kwa kasi kubwa, huku halmashauri 100 zikisuasua.

"Naziagiza hizi halmashauri 100 ziandae maelezo ya kutosha kwanini wasimamizi wake wasihesabiwe kwa kuwa wanakwamisha safari ya nchi kwenda kwenye viwanda na uchumi wa kati kwa kuchelewesha huduma.

"Ninachokiona hapa ni uzembe tu ambao itabidi wahusika wawajibike, kwanini wengine watekeleze kwa wakati na ufanisi wengine wabaki nyuma," alihoji.

Aliwaagiza waratibu kusimamia utekelezaji kwa weledi miradi hiyo, ili kuhakikisha walengwa wanapata huduma bora kwa wakati na kuongeza kasi ya kudhibiti magonjwa hayo kwa kinga na tiba.

Alisema, vita dhidi ya magonjwa hayo itafanikiwa zaidi iwapo kila mmoja atawajibika katika nafasi yake na kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati na ufanisi na taarifa husika zinatolewa kwa wakati na ubora.

"Viongozi wote ngazi ya halmashauri wahusike na utekelezaji wa miradi hii kwa kuwa, siyo suala la wataalamu wa afya pekee bali sekta zote wakiwamo wakurugenzi wa halmashauri, maofisa mipango wa halmashauri na waweka hazina," alisema. Alisisitiza kuwa katika safari ya kuelekea kwenye nchi ya viwanda na uchumi wa kati, sekta ya afya ni mdau mkubwa kwa kuwa, kadri wananchi wenye uhitaji wanavyopata huduma bora za afya kwa wakati ndivyo wanavyoepuka maradhi.



# Korea yavutiwa uwekezaji umeme Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Kampuni ya Kimataifa ya uzalishaji wa umeme unaotumia gesi ya nchini Korea (FCCPP) umesema Zanzibar imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za uwekezaji ikiwamo mazingira bora ya hali ya hewa.

Umesema mazingira hayo yanawapa moyo wa kuanzisha mradi wao unaokuwa ndani ya bahari masafa ya mita 100, umbali wa ardhi unaoambatana na mita 10 chini ya bahari.

Mwakilishi wa kampuni hiyo, Profesa Injoon Suh, alisema hayo wakati timu yake ikitangaza nia yao ya kutaka kuwekeza mradi wao mbele ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Vuga Mjini Zanzibar.

Prof. Injoon Suh, alisema, umeme unaozalishwa na kampuni hiyo unaweza kabisa kutumia gesi asilia inayozalishwa nchini Tanzania kwa kuongezea na ile inayopatikana kutoka Mashariki ya Kati.

Alisema kiwango cha umeme utakaozalishwa na kampuni hiyo yenye uzoefu na utaalamu wa masuala ya nishati ya gesi unafikia megawatts 215 kiwango ambacho ni kikubwa kwa Zanzibar kinachoweza kutosheleza mahitaji yote ya huduma hiyo.

Mwakilishi huyo alisema, mradi huo una garentii ya kufanya kazi katika kipindi cha miaka 25 na baadaye kukabidhiwa kwa serikali. Alieleza kwamba kampuni ya FCCPP ni moja miongoni mwa kampuni 15 zinazofanya kazi kimataifa ndani ya mwamvuli wa kampuni ya kitaifa ya Korea ya VOE Group.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Iddi, alisema mradi wa uzalishaji wa umeme wa kutumia gesi asilia ni muhimu kwa vile umeonyesha mwelekeo kupungua kwa gharama za matumizi ya huduma hiyo.

Balozi Iddi alisema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado ina nia ya kuwa na chanzo kingine cha umeme utakaokuwa mbadala endapo kutatokea hitilafu kwenye chanzo kimoja kilichopo kinachotumika hivi sasa Visiwani Zanzibar kilichoanzia Tanzania Bara.

Aliushauri uongozi wa kampuni ya FCCPP kutayarisha maombi ya kuanzisha mradi na kuyawasilisha serikalini ili kufanyiwa kazi.



Mhandisi Mwandamizi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Victor Kweka, akitoa ufafanuzi kuhusu gari lenye mawasiliano, linavyofanya kazi kwa mabalozi 42 wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali walipotembelea mamlaka hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni wa wiki. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# DC Rajab aahidi usimamizi wa sheria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Rajab Ali Rajab, ameahidi kuwa ofisi yake itaendelea kusimamia sheria na taratibu zilizowekwa kwa kuhakikisha kuwa taratibu hizo hazivunjwi na kukiukwa.

Aliyasema hayo katika Kijiji cha Pangeni, wakati alipofuatilia mgogoro wa shamba la familia ya marehemu Ali Vuaa, linalodaiwa kuuzwa baadhi ya sehemu bila ya kuwashirikisha watu wengine wa familia hiyo.

Alisema atahakikisha sheria za serikali zinafuatwa katika kila jambo ikiwamo kusimamia, kulima au kuuza mashamba.

Alisema shamba lolote la wakfu (mali ya serikali) haliuzwi hivyo ni vyema watu wote wakafuata taratibu.

Aliitaka familia hiyo ikae pamoja na kuelewana katika maandishi na nyaraka zao za shamba ili wafuate yale yaliyoandikwa.

Akizungumzia kuhusu mzozo wa madai ya kuuzwa kwa baadhi ya sehemu, kaka mkubwa wa familia hiyo, Hassan Ali Vuaa, alisema kwa sasa wamekuwa hawafahamu nini anachodai ndugu yao Vuai Ali Vuaa, kwa kuwa kila jambo wanalifanya kwa utaratibu waliokubaliana.

Alisema shamba lao la wakfu hawajauza sehemu yoyote kama taratibu zinavyoelekeza na sehemu ya shamba inayoruhusika kugawana, wamegawana na kuuza na kufanyia shughuli walizojipangia ikiwamo kusomesha watoto.

# Ahimiza usimamizi wa alama za mipaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya kati Unguja, Hamida Mussa Khamis, amewataka wananchi na viongozi mbalimbali wa wilaya hiyo kulinda na kusimamia alama za mipaka zinazowekwa katika maeneo yao ili kujua shehia wanaziongoza.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi, masheha na watendaji wa wilaya hiyo Kijiji cha Ubago, wakati wa uzinduzi wa uwekaji alama inayobainisha Shehia ya Dunga Kiembeni na Kidimni.

Alisema alama hizo hazina lengo la kuwazuia wananchi kuendelea na shughuli zao bali zitawaongoza masheha kutoa huduma kwa wananchi wanaowaongoza kwa urahisi. “Pia alama hizo zitasaidia kuondoa migogoro baina ya upande mmoja na upande mwingine,” alisema. Aliwataka wananchi kutojiingiza katika matatizo yatakayosababisha uharibifu wa alama hizo ambazo zitaathiri shughuli zao na kuwataka masheha kuendelea kutoa huduma kwa wananchi bila ubaguzi.

Naye Sheha wa Shehia ya Kidimni, Bishara Saleh Haji, aliishukuru uongozi na kamati ya uwekaji mipaka na ameihakikishia kamati hiyo, kuwa mipaka hiyo haitakuwa chanzo cha mgogoro kati ya shehia.

“Uwekaji wa mipaka hii hautakuwa chanzo cha migogoro bali zitaongoza katika ufanyaji wa shughuli zao.

Kwa upande wake mtaalamu wa uwekaji mipaka kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Talibu Khatib Shaaban, alisema kazi hiyo ni muhimu kwa taifa, jamii na wadau mbalimbali na kusisitiza kuwa haitohusu mashamba wala mali za watu.

# Ujenzi mradi wa umeme Mto Rufiji wahamasishwa

**Na Futuna Selemani,** KIBAHA

WADAU sekta ya viwanda wameulezea ujenzi wa mradi mkubwa wa kuzalishaji umeme katika Bonde la Mto Rufiji maarufu kama 'Stiegler's Gorge' kama ni dhamira ya kweli ya serikali ya kuijenga sekta ya viwanda nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari kiwandani hapo mwishoni mwa wiki,

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Global Packaging (T) Limited kilichopo Kibaha, mkoani Pwani, Benno Mwitumba, alisema maendeleo ya sekta ya viwanda duniani kote yategemea uwepo wa nishati ya uhakika na hivyo kukamilika kwa mradi wa 'Stiegler's Gorge' kutafanikisha azma ya serikali.

"Kukamilika kwa mradi wa umeme wa Mto Rufiji utakwenda kijibu changamoto ya nishati katika sekta mbalimbali za uchumi ikiwamo ya viwanda hapa nchini na kuvutia zaidi uwekezaji katika sekta hiyo ," alisema Mwitumba.

Mwitumba alipongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa na uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025 kwani matunda yake yameshaanza kuonekana.

"Viwanda vinatumia umeme mwingi sana katika kuendesha mitambo yake hivyo kuwapo kwa umeme wa uhakika ni habari njema kwani itachochea ukuaji wa uchumi na kuleta ustawi wa maisha ya Watanzania," alisema.

Alisema tangu serikali itangaze azma yake ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025, kumekuwa na mwamko mkubwa miongoni mwa wawekezaji hapa nchini na pia ujenzi wa mradi wa umeme wa Rufiji utachochea zaidi.

"Kuwapo kwa nishati ya uhakika kutaongeza uzalishaji viwandani na pia ajira nyingi zitatengenezwa kutokana na uwekezaji katika sekta ya viwanda hali itakayopunguza tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini," alisema.

Mwitumba alisema kiwanda kimeshaajiri zaidi ya wafanyakazi 169 ambao wote ni Watanzania hali ya ajira na kuwajengea uwezo vijana kufanya kazi za viwandani na kuingia katika soko la ushindani wa ajira kutokana na ujuzi wanaopata.

"Tumepata nguvu mpya na tunakwenda kuongeza uzalishaji zaidi na hata kupanua kiwanda kutokana na uhakika wa nishati na miundombinu mingine wezeshi kama barabara ambayo serikali inaendelea kuziboresha kuvutia uwekezaji nchini," alisema Mwitumba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Prof. Damian Gabagambi, ambaye shirika lake ni mmoja wa wanahisa wa kiwanda hicho, alisema kiwanda hicho ni muhimu sana katika mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya kilimo kwa kuzalisha vifungashio. "Kiwanda ni sehemu katika kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo na kupelekea bidhaa za Tanzania kuwa katika hali nzuri kwenye masoko ya ndani ya nje," alisema Prof. Gabagambi.



Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Kisukuru, Bakari Mjema, akizungumza na wanachama wa chama hicho, katika Tawi la Kisukuru B, akiwa katika ziara ya kusikiliza kero za wananchi kama sehemu ya kutekeleza agizo la viongozi wa kitaifa, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Wakulima wadogo wapigiwa debe SADC

**Na Beatrice Moses**

WAKUMA wadogo wametajwa kuwa kundi muhimu la kuleta maendeleo ya haraka katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), lakini miundombinu yao ya kilimo ni duni na wakulima wadogo huonekana ni kundi hatari kibiashara lisiloweza kurejesha mikopo.

Hayo yalibainishwa katika Mkutano wa SADC na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine,

Kwamba kilimo ambayo ndiyo shughuli ya kiuchumi wa kundi hili, kimekuwa kikipokea fedha kidogo na kukwepwa wakati wa uwekezaji. Akichangia majadiliano katika kikao hicho, Justine alisema matokeo ya tabia ya kukinyima kilimo fedha na kukikwepa wakati wa uwekezaji, yamesababisha kuvia kwa maendeleo ya Afrika kwa jumla. "Kilimo ni sekta muhimu katika chumi za SADC, na hivi ndivyo ilivyo kwa bara zima la Afrika," alisisitiza.

Alisema kilimo kinapaswa kutazamwa kwa upana wake na kupewa kipaumbele katika maeneo ya umwagiliaji, maghala, usindikaji, masoko na kadhalika.

Akitumia mfano wa Tanzania, Justine alisema Tanzania ina zaidi ya miradi 2,400 ya umwagiliaji lakini ni kiasi cha asilimia 40 inafanyakazi. Lakini, akaongeza, umuhimu wa kilimo Tanzania unajitokeza vizuri kwa kuangalia yafuatayo:

Kinachangia asilimia 29 ya pato la taifa (GDP), kinatoa asilimia 65 za ajira, kinatoa asilimia 65 za malighafi kwa viwanda na kinachangia asilimia 30 la pato la fedha ya kigeni.

"Mazao muhimu Tanzania ni mazao yenye punje, mifugo, korosho, kahawa, chai, pamba, mkonge, tumbaku, karafuu na miwa. Pamoja na ukweli huu wa wazi kilimo kimeendelea kupewa fedha kidogo na kukosa uwekezaji," alieleza.

Aliwashauri wakulima wadogo wajengewe taratibu za udhamini kwa mikopo ya benki kwa kuwekewa dhamana ya hata kufikia asilimia 50 ili kuondoa dhana ya kwamba ni kundi la kibiashara lisilokopesheka na mikopo yao

iwe na ada (fee) ya asilimia moja kwa mwaka ili mikopo hii iwe ndiyo mikopo ambayo watu wanaweza kuimudu katika soko. Justine alisema iwepo ari ya kuunga mkono mipango, fikira na mawazo ya watu wa vijijini na uwepo moyo wa kukubali kuzijaribu njia, namna, huduma na mipango bunifu au mpya vinavyolenga kubadili maisha vijijini.

## NEMC, TBS wapigilia mifuko ya plastiki

**Na Enock Charles**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEM), na Shirika la Viwango nchini (TBS) wamevionya viwanda na baadhi ya wafanyabiashara ambao wamekuwa wakiingiza na kusambaza mifuko ya plastiki kwa njia za magendo kutoka nchi za jirani kinyume cha sheria.

Wakizungumza na waandishi wa habari baada ya taasisi hizo mbili kuafikiana juu ya hatua za kuchukua, Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hapatakuwa na uvumilivu kwa mtu au taasisi yoyote itakayokiuka katazo la matumizi ya plastiki.

"Tunawaonya watengenezaji, waagizaji kutoka nchi za jirani, wasambazaji na watumiaji kwa ujumla kuheshimu katazo lililotolewa na serikali kuanzia tarehe 1 Juni, 2019 la upigaji marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki, kinyume na hapo sheria itachukua mkondo wake," alisema Dk. Gwamaka. Aliongeza kuwa tayari Baraza limewachukulia hatua baadhi ya watendaji ambao walikuwa wakishirikiana na wanyabiashara kutoka nchi jirani kwa kuwafunguliwa kesi mahakamani na wasambazaji 56 wameshatozwa faini ya shilingi 200,000 kila mmoja.

"Baraza limeshawafikisha wafanyakazi wawili wa TBS jijini Arusha kwa kuwa walishirikiana na wafanyabiashara wasio waaminifu kutoka nchi jirani kuingiza mifuko ambayo hapa nchini imekatazwa na ni kinyume cha sheria," alieleza Dk. Gwamaka.

Aidha, alieleza kuwa hata ofisi zao zilizopo mipakani zimeanza kutoa makucha, kwani huko jijini Mbeya wamefanikiwa kukamata zaidi ya tani 15 ya mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, alieleza vigezo ambavyo vinatumika ili mifuko hiyo iwe na sifa inayotakiwa kuwa ni jina la mzalishaji, 70 GSM pia iwe inaweza kujirejeleza.

"TBS tunatumia vigezo kadhaa ili mfuko uonekane umekidhi vigezo ikiwamo 70 GSM, uwezo wa kujirejeleza pamoja na jina la mzalishaji, na kwa wale wanaoagiza nje ya nchi waangalie vigezo hivyo hivyo na wakishindwa kufanya hivyo mizigo yao itazuiliwa na mamlaka husika," alisema Dk. Ngenya.

## HABARI KIMATAIFA

# Bomu laua watu 63, kujeruhi 180

**KABUL,** Afghanistan

BOMU limelipuka katika ukumbi wa harusi katika mji mkuu wa Afghanistan, Kabul na kuwaua takribani watu 63 na kuwajeruhi zaidi ya 180.

Walioshuhudia waliiambia BBC kwamba mlipuaji wa kujitolea muhanga alijilipua wakati wa sherehe hiyo ya harusi.

Mlipuko huo ulitokea saa nne na dakika 40 saa za Afghanistan katika eneo lililopo magharibi mwa mji ulio na rai wengi Waislamu wa dhehebu la Kishia. Kundi la Taliban limekana kwamba ndilo lililohusika na shambulio hilo. Hakuna kundi jingine lolote lililokiri kutekeleza shambulio hilo.

**Kwa takriban dakika 20 ukumbi huo ulikuwa umejaa moshi.**

Wapiganaji wa Kiislamu kutoka dhehebu la Sunni, ikiwamo kundi la Taliban na kundi la wapiganaji wa Islamic State mara kwa mara wamekuwa wakiwalenga Waislamu wa Hazara wa dhehebu la Shia walio wachache nchini Afghanistan na Pakistan.

Waziri wa masuala ya ndani nchini Afghanistan amethibitisha vifo hivyo saa chache baada ya bomu hilo kulipuka. Picha zilizosambazwa katika mitandao ya kijamii zilionyesha miili ikiwa imetapakaa, huku viti na meza zikiwa zimependukia.

Harusi za Afghanistan huruhusu mamia ya wageni ambao hukongamana katika kumbi kubwa ambapo wanaume hutengwa na wanawake na watoto.

Mgeni mmoja kwa jina Mohammad Farhag alisema kwamba alikuwa katika eneo la wanawake wakati aliposikia mlipuko mkubwa katika eneo la wanaume.

"Kila mtu alikimbia nje akipiga kelele na kulia," alikiambia chombo cha habari cha AFP.

"Kwa takriban dakika 20 ukumbi huo ulikuwa umejaa moshi. Karibu kila mtu katika eneo la wanaume ni aidha wamekufa au kujeruhiwa. Sasa saa mbili baada ya mlipuko, wanaendelea kutoa miili ndani ya ukumbi huo."

Muhudumu mmoja wa chakula, Sayed Agha Shah alisema kwamba kila mtu alikuwa akikimbia baada ya mlipuko huo. **BBC**



Wahudumu wa vituo vya afya wakiwabeba waliojeruhiwa kwa mlipuko wa bomu kuwapeleka hospitali, wakati wa sherehe ya harusi mjini Kabul nchini Afghanistan. **PICHA: BBC**

## Mteja aua mhudumu mgahawani

**PARIS,** Ufaransa

MHUDUMU mmoja wa mgahawa mjini Paris amepigwa risasi hadi kufa na mteja ambaye amedaiwa kwamba alikuwa amekasirishwa kwa kuwa 'sandwich' yake haikuandaliwa haraka iwezekanavyo.

Maofisa wa polisi wanasema kwamba uchunguzi umeanzishwa baada ya tukio hilo siku ya Ijumaa jioni mashariki mwa eneo la Le-Grand. Mshukiwa alitoroka katika eneo hilo na hajapatikana.

Wafanyakazi wa ambulance walijaribu kuokoa maisha ya muhudumu huyo ambaye alikuwa amepigwa risasi katika bega lake, lakini alifariki papo hapo.

Wenzake waliwaambia maofisa wa polisi kwamba mteja huyo alikuwa na hasira katika duka hilo la Pizza na Sandwich kutokana na muda mrefu ambao ilichukua kuandaliwa.

" Inasikitisha", mwanamke mmoja mwenye umri wa miaka 29 alikiambia chombo kimoja cha habari nchini Ufaransa. **BBC**

## Jeshi la UN lashambulia

**RIPOLI,** Libya

UMOJA wa Mataifa umesema leo kuwa kikosi cha kijeshi Mashariki mwa Libya kimeharibu uwanja wa ndege wa kiraia kwa kufanya mashambulizi ya anga katika eneo la Magharibi mwa nchi hiyo.

Wiki iliyopita, kikosi hicho cha jeshi la LNA kilisema kuwa mara mbili kilishambulia uwanja wa ndege wa Zuwara, mji ulioko Magharibi mwa Tripoli kwa mabomu na kusema kililenga jengo la kuegesha ndege linalotumiwa na Uturuki.

Mashambulizi hayo ni sehemu ya kampeni ambayo kwa sasa imeingia miezi wa tano ya kujaribu kuchukuwa mamlaka ambayo yamo mikononi mwa serikali inayotambulika kimataifa.

Kikosi hicho cha LNA kinaongozwa na Khalifa Haftar katika eneo la Mashariki mwa nchi hiyo. **DW**

# Maelfu ya waandamanaji waitega serikali kukusanyika Hong Kong

**HONG KONG,** China

MAELFU ya wakazi wa Hong Kong wamekusanyika katika bustani ya Victoria Park, na kuwabainishia maofisa wa serikali jinsi wanavyoungwa mkono na wananchi na wanaweza kuandamana kwa amani.

Wakazi mbalimbali ikiwamo wazee wa familia wanajiunga na wanaharakati vijana na wengine wenye msimamo mkali katika maandamano hayo. Waandalizi wanakadiria watu wasiopungua milioni mbili wanashiriki katika maandamano hayo, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuwahi kushuhudiwa tangu mwaka 1997 katika maandamano jimboni humo.

Polisi imeruhusu watu wakusanyike lakini wasiandamane. Waandamanaji wameipuuza amri hiyo, wameteremka kwa wingi kati kati ya Jiji la Hong Kong licha ya mvua kali.

"Ikiwa mbinu za Beijing na Hong Kong ni kuona vuguvugu letu linadhoofika, wamekosea..."hatutochoka." amesema Bonnie Leung wa shirika linalopigania haki za raia-CHRF.

Waandamanaji wanasema wamepania kuionyesha serikali hawatoachilia mbali madai yao matano ikiwa ni pamoja na kubatilisha muswaada wa sheria kuhusu kuhamishiwa China wahalifu na uchunguzi huru, kuhusu matumizi ya nguvu ya polisi. Waandamanaji wanadai pia kiongozi wa serikali ya jimbo hilo Carrie Lam ajiuzulu.

"Tutabakia hapa hapa, tutasimama kidete hadi watujibu. Kwa pamoja tuna nguvu zaidi," anasema mwanafunzi Harles Ho. Kijana huyo wa miaka 20 anasema mvua kali haitobadilisha msimamo wao.

Katika wakati ambapo matumizi ya nguvu yalighubika maandamano yao mnamo wiki za hivi karibuni, maandalizi ya maandamano ya leo yanatarajiwa kudhihirisha kuwa wakazi wa Hong Kong wanaweza kuandamana kwa amani.

Waandamanaji shupavu walikosolewa wiki hii baada ya maandamano katika uwanja wa ndege wa kimataifa kumalizikia kwa mapigano dhidi ya polisi wa kuzuia fujo. Waandamanaji hao waliwazuia abiria wasisafiri na baadaye kuwavamia watu wawili waliokuwa wakiwatuhumu kuwa majasusi wa Serikali Kuu ya China.

Vuguvugu la maandamano limeanza Juni 9 iliyopita katika jimbo hilo la Hong Kong lililokuwa zamani likisimamiwa na Uingereza. **DW**

# Waliofariki dunia ajali ya lori Morogoro wafikia 95

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya watu waliopoteza maisha kufuatia ajali ya moto wa lori la mafuta iliyotokea Morogoro Agosti 10, imeongezeka na kufika 95 baada ya majeruhi mwingine aliyekuwa amelazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kufariki dunia jana.

Kufuatia vifo hivyo, idadi ya wagonjwa waliobaki ni 20 kati ya 46 waliokuwa wamefikishwa Muhimbili kupatiwa matibabu.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MNH, Aminiel Aligaesha, alimtaja aliyefariki dunia kuwa ni Rajabu Ally (32).

Pia majeruhi mwingine kutoka Morogoro alifikishwa hospitalini hapo jana mchana baada ya kupata rufani.

Aligaesha alisema kwa sasa majeruhi wamebaki 20 na wote wako katika wodi ya uangalizi maalum (ICU).

Alisema madaktari wanaendelea kufanya jitihada kuokoa maisha ya majeruhi hao. Mkuu huyu wa mawasiliano alisisitiza watu kuendelea kuchangia damu kwa ajili ya majeruhi hao na wagonjwa wengine wenye uhitaji.

Idadi hiyo ya waliopoteza maisha inatokana na ajali ya lori lililokuwa limebeba tangi la mafuta ya petroli, kuanguka eneo la Msamvu mkoani Morogoro na baadaye kulipuka wakati baadhi ya wananchi wakichota mafuta yaliyokuwa yanamwagika.



Sehemu ya Barabara ya Samora, ikiwa imefungwa kwa ajili ya maonyesho ya nne ya bidhaa za wajasiriamali yanayoendelea, jijini Dar es Salaam jana, ambayo yamekuwa fursa wakati wa mkutano wa SADC. **PICHA: JOHN BADI**

## Serikali yaagiza kampuni kulipa ushuru

INATOKA UK. 5

Geita kwa kuongoza kitaifa katika ukusanyaji wa fedha nyingi na usimamizi mzuri wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Pia aliipongeza GGM kwa kusaidia kutekeleza miradi mbalimbali ya jamii katika halmashauri zote za Mkoa wa Geita na kuongeza kuwa GGM imekuwa ni kinara katika uchangiaji wa mapato na katika mambo mengi mazuri, na yote haya ni kutokana na juhudi zilizofanywa kutokana na ushirikiano kati ya GGM na Serikali ya Mkoa wa Geita.

Gbriel alibainisha kuwa tangu soko kuu la dhahabu lifunguliwe katika halmashauri hiyo mkoani Geita, halmashauri hiyo imekusanya zaidi ya Sh. milioni 200 zilizotokana ushuru wa huduma, na kuwa hiyo imetokana na usimamizi makini kwenye soko la dhahabu, mkuu huyo aliwashukuru viongozi wa Mkoa wa Geita na kuwataka kujenga uvumilivu maana kwenye fedha kuna lawama na maneno mengi, na kuwaambia kuwa iwapo kuna mtu ana taarifa zozote za matumizi mabaya ya fedha za umma aziwasilishe Takukuru kwa uchunguzi.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa GGM, Richard Jordinson, alisema kuwa kampuni hiyo imepanga kutumia kiasi cha shilingi za bilioni 9.2 kutekeleza miradi ya kijamii kwa jamii zinazozunguka mgodi mpango kazi wa mwaka 2019/2020.

"Tunajivunia mafanikio haya makubwa na tunaamini katika kufanya kazi pamoja na jamii inayotuzunguka ili kuwa na uwajibikaji pamoja na kutekeleza na kutimiza miradi ya yetu yenye kuleta tija kwa jamii," alisema Jordinson.

Alisema kuwa GGM imetia saini hati ya makubaliano na halmashauri hizo kuashiria mwanzo wa utekelezaji wa miradi ya jamii kwa mwaka 2019 chini ya mpango wa kampuni wa uwajibikaji katika jamii kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mbalimbali afya, mazingira, elimu, kilimo na miundombinu.

Pia aliongeza kuwa kampuni hiyo inakusudia kuacha alama na thamani kwa wadau na wakazi wa Mji wa Geita na Taifa kwa ujumla kupitia uchimbaji wa madini ya dhahabu uwekezaji wa moja kwa moja, ajira na kodi zitokanazo na mapato yanayopatikana kupitia sekta ya madini.

Jordinson alisema kampuni hiyo itaendelea kuunga mkono jitihada za serikali ya Tanzania kwa kutekeleza miradi endelevu katika maeneo ya kimkakati yaliyoainishwa na mpango wa serikali wa miaka mitano dira ya maendeleo ya mwaka 2025 na malengo endelevu ya mwaka 2030 pia kampuni hiyo itaendelea kushirikiana na halmashauri za Geita pamoja na jamii inayozunguka GGM.

## Lori mafuta lateketea, laua, kujeruhi dereva

INATOKA UK. 5

kwenye mchanga, huku anawaka moto mwilini, lakini konda wake alikuwa ameshapoteza maisha," alisema Shija. Naye dereva wa gari hilo, Ibrahimu Issa, alisema ajali hiyo ilitokea wakati akimkwepa dereva wa gari dogo aina ya Toyota Voltz, ambaye alikuwa anajaribu kupita bila ya kuchukua tahadhari na kusababisha gari hilo kuanguka mtaroni na kuwaka moto papo hapo.

Hata hivyo, alisema baada ya gari kuanguka liliwaka moto kisha kuvunja kioo cha mbele cha gari na kuruka, na kwamba alipofika chini alivunjika mguu wa kushoto na kuanza kujigalagaza kwenye mchanga kuzima moto, na kuongeza kuwa utingo wake alipoteza maisha.

Kamanda wa Zimamoto na Uokoaji, Duma Mhamedi, alisema ili kuzuia majanga ya moto, ni vema wananchi wawe wanatoa taarifa kwa wakati, na kuacha tabia ya kupiga picha kwa kutumia simu na kusambaza mitandaoni.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, na kusema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa gari dogo kuendesha kwa mwendokasi, ambaye alilipita lori lilo na kisha kuligonga kwa nyuma.

## Mwanafunzi ajiua kwa risasi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWANAFUNZI wa kidato cha pili Shule ya Sekondari Meru ya jijini Arusha, Faisal Ibrahimu (19), mkazi wa Kata ya Kati mkoani Arusha, amejiua kwa kujipiga risasi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema mwanafunzi huyo alijipigia risasi ya bunduki aina ya Rifle Winchester, mali ya baba yake Salim Ibrahimu (56).

"Majira aliyojiua Agosti 18, mwaka huu, saa 11: 00 alfajiri, ambapo alijipiga kwenye paji la uso akiwa chumbani kwake kwenye nyumba za Shirika la Nyumba za Taifa zilizopo eneo la soko kuu katika Kata ya Kati wanakoishi na wazazi wake," alisema.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni msongo wa mawazo uliotokana na matumizi ya dawa za kulevya.

Shana alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa Mount Meru ukisubiri uchunguzi zaidi wa madaktari.

Alitoa wito kwa kampuni, taasisi na watu binafsi kutumia silaha kwa umakini na sehemu sahihi ili kuepusha madhara.

Alisema watawafutia umiliki watu wote watakaotumia silaha kinyume cha utaratibu na watakaobainika kushindwa kuzitunza kwa usahihi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za Kazi**
Anahitajika - Mhasiibu
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma
Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533

**NIPASHE NI JIBU LAKO**
NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

## PLOTI HEKARI MBILI INAUZWA MTONI KIJICHI-WILAYA YA TEMEKE

**Ploti hekari mbili inauzwa Mtoni**
Kijichi-wilaya ya temeke inafaa kwa biashara yeyote kubwa inafaa kwa kanisa na msikiti.

**Mawasiliano namba : 0778 742 848**

115375702

## KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**AZAN SAID SALUM** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI T 323 BMH YENYE CHASSIS NO 5118068 NA ENGINE NO 6245899 TAARIFA YA POLISI KAH/TR/RB/621/2019 NA GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI T 243 BMH CHASIS NO 5118090 NA ENGINE NO 6245931

KWA YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI:
**KAH/TR/RB/622/2019**

xxxxxx

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**WUZHOU ANATANGAZA** KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA HONLOG YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 359 CCK CHASSIS NO * LJEPCJL67JA01630*
A ENGINE NO 157FMI*JXA53314

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
**KGG/RB/312/2019**

xxxxxx

*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

# Nipashe

www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

## NEWSPAPER

**CLASSFIED ADVERTISEMENT**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# COUTINHO ATUA BAYERN MUNICH

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich wamethibitisha usajili wa kiungo wa Brazil, Philippe Coutinho kutoka Barcelona.

Nyota huyo aliwekwa nje ya kikosi cha Barcelona kilichocheza na Athletic Bilbao kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, usiku wa juzi kwa sababu alikuwa akihusishwa na kuachana na timu hiyo na hatimaye Bayern imethibitisha kumnasa.

Kiungo mshambuliaji huyo wa zamani wa Liverpool amejiunga na Bayern Munich kwa mkopo wa msimu mmoja wenye makubaliano ya kumnunua jumla. Katika taarifa ya Bayern Munich iliyotumwa kwenye Twitter ya klabu hiyo, ilisomeka hivi: "FC Bayern na FC Barcelona zimefikia makubaliano ya kimsingi kwa ajili ya usajili wa Coutinho kwa mkopo, huku kukiwa na kipengele cha kumsajili jumla. Mambo mengine yatafuata."

Coutinho anatazamiwa kutua Munich siku chache sijazo kwa ajili ya kukamilisha vipimo vya afya na kusaini mkataba rasmi katika klabu yake mpya.

Mwenyekiti wa klabu ya Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge alisema: "Jina halijalishi, kinachojalisha ni uwezo. Tumekuwa tukimfuatilia kwa muda sasa."

Kwenye kipindi chote cha dirisha hili la majira ya joto, Coutinho amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwenye kikosi hicho cha Liverpool kabla ya sasa kuthibitishwa atakwenda kukipiga Bundesliga msimu huu.

# Kaka afunguka Pogba kuondoka Man United

**LONDON,** England

KAKA wa mchezaji wa Manchester United, Paul Pogba, Mathias Pogba amedai lolote linaweza kutokea kuanzia sasa hadi dirisha kubwa la uhamisho litakapofungwa kwingineko barani Ulaya na mdogo wake anasubiri ofa ya Real Madrid.

Hata hivyo, Mathias amesisitiza mdogo wake ataendelea kuitumikia Manchester United kwa moyo mmoja akitolea mfano wa nyota wa PSG, Neymar ambaye anasubiri uhamisho wa kurudi Hispania huku akitakiwa na Barcelona na Real Madrid.

Man United imeendelea kusisitiza haina mpango wa kumuuza staa huyo wa kimataifa wa Ufaransa ambaye mwanzoni mwa dirisha lililofungwa akiwa nchini Japan alidai kwamba anataka kupata changamoto mpya nje ya Manchester United.

Staa huyo wa kimataifa wa Ufaransa moja kati ya ndoto zake ni kucheza katika klabu ya Real Madrid akipigiwa upatu na Kocha Zinedine Zidane ambaye anamtaka staa huyo kwa nguvu zote.

Man United inaweka ngumu kumtoa Pogba kwa sababu kwa sasa haitaweza kusajili mchezaji yeyote wa kuziba pengo lake baada ya dirisha la Uingereza kufungwa.





# Pochettino: Eriksen ataondoka Spurs

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, ameweka wazi wanaweza kumkosa mchezaji wao, Christian Eriksen ndani ya mwezi huu.

Spurs wamemwekea Eriksen ofa mpya ya mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, lakini kiungo huyo ameweka wazi bado hayupo tayari kuanza mazungumzo ya mkataba mpya. Pochettino alisema lolote linaweza kutokea kwa sababu si yeye ambaye anataka liwe, lakini muda mwingine lazima mambo yafanyike.

"Bado tunatakiwa kusubiri mpaka Septemba 22, hakutakuwa na mabadiliko makubwa ambayo yataleta matatizo kwetu, tunaweza kubadilisha mawazo na mchezaji akabadilisha mawazo yake, kwa muda huu ni ngumu kusema moja kwa moja tusubiri Septemba ifike," alisema.

Aliongeza timu yake bado haijatulia kama ambavyo anataka iwe, lakini bado anafanyia kazi ili kuhakikisha suala hilo linakamilika ifikapo Septemba 2.

## HABARI MICHEZO

# Sancho agombewa Man Utd, City

**LONDON,** England

MCHEZAJI Jadon Sancho ameripotiwa kwamba ataachana na Borussia Dortmund mwishoni mwa msimu huu na jambo hilo limedaiwa kwamba tayari limeshaanza kuwaingiza vitani wababe wawili wa Ligi Kuu England, Manchester United na Manchester City wakiwania saini yake.

Taarifa za kutoka Ujerumani zinadai kwamba Dortmund wameshaanza mchakato wa kutafuta mbadala wa Mwingereza huyo baada ya kukubaliana na ukweli kwamba atawaacha mwishoni mwa msimu.

Kwa mujibu wa Daily Mail, Sancho ataigharimu timu itakayohitaji saini yake zaidi ya pauni mlioni 100.

Man United walihitaji huduma ya winga huyo wa Kingereza na walijaribu kufanya hivyo kwenye dirisha la kiangazi huko Ulaya kabla halijafungwa upande wa England.

Man City nao wamekuwa wakimfuatilia kwa karibu mchezaji huyo aliyewahi kuwa kwenye kikosi chao kabla ya kumpiga bei kwenda Dortmund kwa pauni milioni saba mwaka 2017.




# SOLSKJAER ATAKA SANCHEZ ABAKI UTD




**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema kuwa anataka mshambuliaji wake, Alexis Sanchez abaki ndani ya kikosi hicho.

Solskjaer awali alikuwa anaonekana kutokuwa na mpango na mchezaji huyo ambaye tangu kutua pale Old Trafford akitokea Arsenal ameshindwa kuwika.

Sanchez amekuwa akihusishwa na kuwaniwa na timu za Italia na inaonekana hana nafasi ya kucheza ndani ya kikosi cha kwanza United.

Dirisha la Ulaya litakavyofungwa Septemba 2 na huenda likamhusu licha ya mshahara kuwa kikwazo.

"Alexis ni mchezaji mzuri, ana weledi amerejea kufanya kazi na sisi ni sehemu ya kikosi chetu na tuna mpango naye, hatuna washambuliaji wengi, hivyo atatufaa ndani ya kikosi," alisema.

# Mo Salah kuweka rekodi ya mshahara

**LIVERPOOL,** England

KLABU ya Liverpool imeripotiwa kutaka kumfanya supastaa wao, Mohamed Salah kuwa mmoja wa wanasoka wanaolipwa mshahara mkubwa kwenye Ligi Kuu ya England.

Wakifahamu wazi kwamba mshambuliaji wao huyo huu unaweza kuwa msimu wa mwisho kucheza kwenye Ligi Kuu England na kisha kuondoka mwakani, Liverpool sasa wamepanga kumbakiza kwa ushawishi wa kutumia fedha.

Kinachoripotiwa ni kwamba wakali hao wa Anfield wamepanga kumpa Mo Salah mshahara wa pauni 430,000 kwa wiki ili aendelee kubaki kwenye kikosi chao kwa muda mrefu.

Salah amekuwa mmoja wa vinara wa mabao kwenye Ligi Kuu England tangu alipojiunga na Liverpool mwaka 2017, akishinda Kiatu cha Dhahabu kwa misimu yote miwili iliyopita, akifunga mabao 72 katika mechi 107 alizocheza kwenye michuano yote.

Kwa mujibu wa The Sun, Real Madrid wameonyesha dhamira ya dhati ya kuhitaji saini ya mshambuliaji huyo na walitaka kumnasa kwenye majira haya ya kiangazi kabla ya kuamua kuliweka kando jambo hilo wakisubiri dirisha la majira ya kiangazi la mwakani.

Mkataba wa sasa wa Salah na Liverpool, alisaini tena mwaka 2018, lakini wababe hao wanataka kumboreshea zaidi mshahara wake ili asishawishike kuhama Anfield. Jioni ya juzi Jumamosi, Liverpool walitarajia kumenyana na Southampton huko St Mary's kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, huku wakiwa na mzuka wa kutoka kuichapa Chelsea kwenye UEFA Super Cup Jumatano iliyopita.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ZIDANE: SITAKI TENA BALE AONDOKE REAL

Gareth na kila mmoja hapa anakwenda kuonyesha thamani ya jezi ya klabu hii na anastahili...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesema kwamba Gareth Bale "atabakia" Real Madrid baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales kumtengenezea bao la ufunguzi Karim Benzema wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Celta Vigo juzi, Jumamosi.

Bale alianzishwa kwenye mchezo huo baada ya kuhusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo kipindi hiki cha majira ya joto, lakini Zidane alisisitiza kwamba mara zote alikuwa na mpango wa kumchezesha Bale.

"Atabakia na wote tunafikiria kuhusu jambo hilo ambalo ni chanya kwetu," alisema Zidane.

"Majeraha kwa Eden Hazard ilikuwa ya bahati mbaya kwetu, lakini hakikubadilisha mpango wa kumtumia Bale.

> "Gareth na kila mmoja hapa anakwenda kuonyesha thamani ya jezi ya klabu hii na kuonyesha kwa nini anastahili kuivaa."

Bale alishamjaribu golikipa wa Celta, Ruben Blanco kwa shuti kali kabla ya kumtengenezea pande zuri Benzema ambaye alifunga bao dakika ya 12.

Celta walijibu haraka mashambulizi na walionekana kama wangesawazisha, lakini bao la Brais Mendez lilikataliwa na teknolojia ya maamuzi ya video.

Toni Kroos aliongeza bao la pili kwa Real akifunga kwa shuti kutoka umbali wa yadi 25, muda mfupi baada ya Luka Modric kutokewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumchezea vibaya Denis Suarez.

Baada ya kubakia wachezaji 10 kwenye dimba la Municipal de Balaidos, Real walifunga bao la tatu wakati Lucas Vazquez alipomalizia vizuri pasi ya dakika za mwisho.

Bao la kufutia machozi kwa Celta lilifungwa na Iker Losada aliyetokea benchi, baada ya kumzidi akili golikipa, Thibaut Courtois.

Mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, Barcelona walipoteza kwenye mchezo wao wa kwanza Ijumaa baada ya kufungwa bao 1-0 na Athletic Bilbao.

## ZISIKUPITE

### INTER YAJIAMINI KWA SANCHEZ

INTER Milan inatumai kuinasa saini ya mshambuliaji Alexis Sanchez kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu na inajiamini itakubaliana mpango huo na Manchester United na tayari miamba hiyo ya Old Trafford imemruhusu mchezaji huyo kufanya mazungumzo na Waitaliano hao. ***(Mail on Sunday)***

### ERIKSEN AANDALIWA DAU REAL

REAL Madrid itatoa ofa ya pauni milioni 60 kwa kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen. Mdenmark huyo mwenye umri wa miaka 27, anaweza kuondoka kabla ya dirisha la usajili Hispania kufungwa Septemba 2, mwaka huu. ***(Sun on Sunday)***

### MADRID KUMRUDIA POGBA

REAL Madrid inajiandaa kujaribu bahati yao ikitumia uhusiano wa Paul Pogba, 26, na Manchester United katika mpango wao wa kuendeleza lengo la kuipata saini ya kiungo huyo Mfaransa. ***(Sunday Times)***

### COUTINHO KUIJAZA NOTI LIVER

LIVERPOOL inaweza kuingiza pauni milioni 18 kama mshambuliaji wao wa zamani Mbrazil Philippe Coutinho, 27, atajiunga na Bayern Munich kwa mkopo akitokea Barcelona. ***(Mail on Sunday)***

### STURRIDGE NJIA PANDA

DANIEL Sturridge, yupo katikati ya vita ama ajiunge na Trabzonspor ya Uturuki au Monaco ya Ufaransa. Nyota huyo wa England ni mchezaji huru tangu aachwe na Liverpool Juni mwaka huu. ***(Sunday Express)***

### EVERTON YAITIWA RIBERY

EVERTON imepewa ofa ya kumsajili winga wa zamani wa Ufaransa, Franck Ribery, 36, ambaye yupo huru baada ya kuondoka Bayern Munich baada ya kuitumikia miamba hiyo ya Bundesliga kwa miaka 12. ***(90Min)***

### SANCHES KUTIMKA BAYERN

KIUNGO Mreno Renato Sanches, anataka kuondoka Bayern kwa kukosa nafasi. ***(Sport1 - in German)***

### OZIL MLANGO WAZI DC UTD

MESUT Ozil, 30, bado anaweza kuondoka Arsenal na kujiunga na DC United kama miamba hiyo ya Ligi Kuu Marekani (MLS), inaweza kufanikisha uhamisho huo. ***(Daily Star Sunday)***

### BALOTELLI HAKIJAELEWEKA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester City na Liverpool, Mtaliano Mario Balotelli, 29, yupo katika hatihati ya kujiunga na klabu ya Brescia ya Serie A. ***(La Gazzetta, via Sun)***

### BOATENG AFUNGUKA UNITED

KIUNGO wa Barcelona na Ghana, Kevin-Prince Boateng, 32, amesema angeweza kuichezea Manchester United kwa miaka 10 kama mtazamo wake ungekuwa mzuri tangu awali katika wasifu wake kikazi. ***(Goal)***

### BOLASIE AWANIWA UTURUKI

WINGA wa Everton, Yannick Bolasie, 30, yupo tayari kuondoka hapo Goodison Park, wakati huu miamba ya Uturuki, Besiktas na Trabzonspor ikivutiwa na nyota huyo wa kimataifa wa Congo. ***(Sun on Sunday)***

HABARI MICHEZO

## Uganda U-15 wadaiwa vijeba

**Na Mwandishi Wetu,** ASMARA

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 3-0, kikosi cha Uganda U-15 huenda kikakutana na adhabu baada ya Ethiopia kuwasilisha malalamiko kuwa wapinzani wao hao walichezesha wachezaji wenye umri mkubwa.

Taarifa kutoka katika Kamati ya Mashindano ya Baraza la Soka la Afrika Mashariki na Kati zimeeleza kuwa imepokea malalamiko kutoka kwa Ethiopia na inayafanyia kazi kabla ya kutoa uamuzi kuhusu rufani hiyo.



Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano hayo, Doris Petra, alisema wachezaji wa Uganda ambao wamedaiwa kuwa na umri mkubwa, hawatasimamishwa, lakini watakapobainika kwamba wamedanganya umri, hatua kali zitachukuliwa.

Petra alisema kuwa kamati yake haitakaa kimya kwa udanganyifu huo, na inajipanga kuchukua hatua kwa timu zote ambazo zimeleta wachezaji wakubwa katika michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza.

"Tumepokea malalamiko haya, tunayafanyia kazi kwa kushirikiana na Kamati ya Utendaji ya Cecafa, tunaamini uamuzi utafanyika kwa kuzingatia kanuni na sheria za mashindano haya, tunajua viongozi walikubaliana kuleta wachezaji watoto kwa ajili ya kufikisha malengo yetu ya kuendeleza soka katika ukanda wetu," alisema kiongozi huyo.

## Mtibwa: Lipuli bado haisomeki

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Mtibwa Sugar limesema mchezo wao wa kwanza wa Ligi Kuu Bara msimu huu dhidi ya Lipuli FC utakuwa mgumu kwa kuwa hawakubahatika kuwasoma kwa namna yoyote wala kubaini aina ya nyota wapya waliowasajili.



Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila (pichani), alisema, mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani, kutokana na kwamba hajausoma aina ya uchezaji wa Lipuli, pamoja usajili walioufanya.

"Mchezo wetu na Lipuli utakuwa mgumu kwa sababu sijaona usajili wao vile vile sijabahatika kuwaona wakicheza mchezo wa kirafiki," alisema Zuberi.

# USAJILI SPRITE BBALL KINGS 2019 'WATETEMESHA' DAR

**Na Mandishi Wetu**

MICHUANO ya Sprite Bball Kings 2019, inatarajiwa 'kutetemesha' medali ya michezo nchini, baada ya timu kibao kujitokeza kujisajili kwa ajili ya kushiriki kinyang'anyiro hicho kinachoandaliwa na EATV, EA Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite.

**Wakati wa ufunguzi wa michuano hiyo, uliofanyika Jumamosi iliyopita katika viwanja vya Mlimani City, jumla ya timu 39 zimejisajili ushiriki michuano hiyo inayotarajiwa kutimua vumbi hivi karibuni huku zoezi hilo la usajili likitarajiwa kuendelea tena leo.**

Aidha, wimbo maalum wa michuano ya Sprite Bball Kings 2019 ulioandaliwa na G Nako 'Warawara', Frida Amani na Chemical, ulizinduliwa Jumamosi mbele ya wageni waalikwa na mamia ya watu waliojitokeza.

Akifungua rasmi michuano hiyo ambayo huu ni msimu wa tatu kufanyika, mwakilishi kutoka Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Malinde Mahona, alisema serikali inatambua juhudi kubwa zinazofanywa na East Africa Tv, East Africa Radio na Kampuni ya Coca-Cola kupitia kinywaji chake cha Sprite kwa moyo wao wa kujitolea kukuza mpira wa kikapu nchini.

"Serikali ipo pamoja na nanyi, inatambua faida kubwa iliyopo kwenye michezo ndio maana inapoona watu wenye moyo kama Coca-Cola, East Africa Radio & East Africa Tv. Tunatoa pongezi sana," alisema Mahona.

"Pia tunawaomba wadau wengine wawekeze katika viwanda vya michezo ili tupate vijana ambao taifa zima linawaangalia, kwa hiyo kwa sasa vijana onyesheni vipaji vyenu katika mashindano haya."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Umma na Mawasiliano wa Coca-Cola ambayo inazalisha kinywaji cha Sprite, Haji Mzee Ally, alisema: "Ahadi yetu kama Coca-Cola ni kuendelea kuwa mstari wa mbele hasa linapokuja suala la kuwasaidia vijana, katika kuendeleza vipaji vyao ambavyo vitaleta mabadiliko katika maisha yao.

"Tumelidhihirisha zaidi kupitia majukwaa mengine ya kuibua vipaji kama vile Coke Studio Afrika, East Africa Got Talent na mashindano ya Copa Coca-Cola."



Baadhi ya wachezaji wakiwa wamevalia uzi mpya wakati wa uzinduzi wa msimu wa tatu wa mashindano ya mpira wa Kikapu ya Sprite Bball Kings 2019 yaliyozinduliwa viwanja vya Mlimani City jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# *Tanzania U-15, Uganda kazi ipo leo*

**Na Somoe Ng'itu,** ASMARA

TIMU ya Soka ya Taifa ya umri chini ya miaka 15 (U-15), inatarajia kuanza kampeni ya kuwania ubingwa wa mashindano ya vijana ya Afrika Mashariki na Kati kwa kuwavaa yosso wenzao kutoka Uganda katika mechi ya Kundi B itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea.

Uganda itashuka uwanjani leo ikiwa na morali wa ushindi wa mabao 3-0 katika mchezo wake wa kwanza dhidi ya Ethiopia wakati Tanzania inashuka dimbani kwa mara ya kwanza katika michuano hii.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Kocha Mkuu wa timu ya Tanzania, Maalim Saleh, alisema kikosi chake kimejiandaa vema na kiko tayari kwa mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 10:30 jioni.

Saleh alisema amewaandaa vijana wake kuonyesha vipaji walivyonavyo katika mashindano haya ambayo malengo yake ni kuendeleza soka katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kocha huyo alisema hana majeruhi katika kikosi chake na kila mchezaji yuko sawa kimwili na kiakili kwa ajili ya kuwavaa wapinzani wao, Uganda.

"Tunamshukuru Mungu tuko salama, tumekuja kwa ajili ya kufanya vema na kuwapa nafasi wachezaji wetu kuonyesha uwezo wao, tumejiandaa kufanya vizuri dhidi ya wapinzani wetu Uganda," alisema kocha huyo.

Naye nahodha wa timu hiyo, Awadh Juma, alisema wachezaji wote wa timu hiyo wako tayari kwa ajili ya kupeperusha vema bendera ya Watanzania katika mashindano hayo.

"Mimi kama nahodha wa timu hii nasema tumejiandaa vizuri, tumejipanga kufanya vizuri katika mechi yetu dhidi ya Uganda, tunawaahidi Watanzania hatutawaangusha," alisema nahodha huyo.

Mechi nyingine ya Kundi B katika mashindano hayo itakayochezwa mapema leo mchana itakuwa ni kati ya yosso wa Sudan Kusini dhidi ya wenzao kutoka Ethiopia.

Mashindano hayo yanayoshirikisha nchi 10 yataendelea tena kesho kwa Kenya kuikaribisha Burundi wakati Sudan itawavaa wenyeji Eritrea ambao walikubali kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Burundi katika mechi ya ufunguzi.

Michezo

Jumatatu Agosti 19, 2019

Nipashe




Zidane: Sitaki tena Bale aondoke Real UKURASA 30



Mwekezaji wa Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, akisherehekea na wachezaji wa timu hiyo kwa kunyanyua juu Ngao ya Jamii baada ya timu hiyo, kuitwaa juzi kwa kuifunga Azam FC mabao 4-2 kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Taifa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simba: Sasa tukutane kwa Mkapa Jumapili

●●● Wakati mashabiki wakihesabu taji la kwanza, Aussems aahidi kufanya kweli huku akieleza...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuanza msimu kwa Ngao ya Jamii kufuatia kuichapa Azam FC mabao 4-2, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wamesema kazi ndiyo imeanza na kuwaita mashabiki wake kujitokeza kwa wingi Uwanja wa Taifa Jumapili kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji.

Simba ambayo imetwaa Ngao hiyo ya Jamii kwa mara ya tatu mfululizo na ya tano kwa ujumla wake, ilipata mabao yake kupitia kwa Msudan, Sharaf Eldin Shiboub aliyefunga mawili kipindi cha kwanza kabla ya viungo wenzake, Mzambia Clatous Chama na Mkenya Francis Kahata kuongeza mawili kipindi cha pili.

Hiyo inakuwa mara ya tano kwa Simba kutwaa Ngao ya Jamii, baada ya mwaka jana wakiichapa Mtibwa Sugar 2-1, mwaka 2011 wakiifunga Yanga 2-0, mwaka 2012 wakiifunga Azam FC 3-2 na mwaka 2017 wakiwafunga tena mahasimu wao wa jadi, Yanga kwa penalti 5-4 baada ya sare ya 0-0.

**Jumapili Simba itashuka dimbani katika mchezo wao wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa ikiwa na kumbukumbu ya kulazimisha sare tasa ugenini kwenye mechi ya awali iliyopigwa Beira, Msumbiji.**

Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems alieleza kuwa sasa akili yake ni katika mchezo dhidi ya UD Songa na kwamba maandalizi tayari yameanza akipania kuibuka na ushindi wa kishindo.

"Uzuri ni kwamba tutakuwa katika uwanja wetu mzuri wa nyumbani na mbele ya mashabiki wetu, maandalizi yanakwenda vizuri na tunaweza kufanya vizuri.

"Mipango dhidi ya Azam itakuwa tofauti na hata kikosi, hivyo mabadiliko ni lazima yafanyike," alisema.

Kwa upande wa Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema, kinachotakiwa kwa sasa ni mashabiki kujitokeza kwa wingi.

Alisema vijana wameonyesha uwezo mkubwa katika mchezo uliopita, hivyo kinachofuata sasa ni dhidi ya UD Songo Taifa Jumapili.

"Kikosi kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi ya Jumapili, mashabiki mjitokeze kwa wingi kuwapa sapoti wachezaji wetu," alisema.

## Zahera aponda kambi ya Yanga

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuwanyong'onyesha mashabiki wake kwa kuchapwa mabao 2-0 dhidi ya Polisi Tanzania siku ya Ijumaa, jana Yanga ilirejeshea furaha kwa kuibanjua AFC Leopars ya Kenya bao 1-0 kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyochezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, huku Kocha Mwinyi Zahera akiponda timu kuweka kambi huko.

Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa Yanga kupata ushindi huo na ilibidi isubiri dakika saba kabla ya mechi kumalizika, ndipo mamia ya mashabiki wa timu hiyo walipopagawa kwa furaha hadi mwisho wa mchezo.

Alikuwa ni Mkongomani Papy Tshishimbi aliyepeleka furaha Jangwani alipofunga bao pekee kwa kichwa akiunganisha mpira wa kona uliopigwa na Patrick Sibomana.

Hali ya uwanja pia haikuwa rafiki kwa timu zote kuonyesha soka safi na badala yake zililazimika kutumia mipira mirefu.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zahera ameponda maandalizi hayo na kusema kuwa ilikuwa ni kupoteza muda bure.

"Tungeweza kuja Moshi na Arusha kucheza mechi kama hakuna matayarisho yoyote ile ya kimataifa kwa sababu huwezi kujiandaa kwenye viwanja vibovu kama hivi ni kupoteza wakati tu," alisema.

Alisema kuwa kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Township Rollers watacheza kwenye kiwanja kizuri, hivyo anatarajia kuwa hawawezi kucheza kwa kiwango cha chini kama walivyocheza mechi hizo mbili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002